

**11 NOVEMBA, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 11 Novemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtakuwa mmeona kwenye Orodha ya Shughuli za Leo kwamba tungeanza na Hati za Kuwasilisha Mezani. Katika Hati za Kuwasilisha Mezani, ipo hapa hati ambayo ilipaswa kuwasilishwa na Waziri wa Afya na akifuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Sasa hati hii haitawasilishwa leo hapa mezani kwa sababu Bunge pamoja na Serikali tunaendelea na mashauriano juu ya mambo ambayo hatujaafikiana vizuri. Kwa hiyo, Bunge hili halitautazama ule muswada ambao ulikuwa umesomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge lililopita na ukapelekwa kwenye Kamati yetu ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa na ratiba tuliyokuwanayo ilikuwa uingie leo hapa Bungeni kwa ajili ya mjadala, lakini pia kumaliza kazi ya kutunga sheria.

Sasa kwa sababu nimeeleza hapo kwamba tunaendelea na mashauriano basi kuna hoja kadhaa ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini zingine wameibua wadau mbalimbali ambao walijitokeza mbele ya Kamati na zingine Serikali inaendelea kuzitazama namna bora ya kuwahudua wananchi kwenye eneo hili la Bima ya Afya. *(Makofi)*

Kwa maelezo hayo muswada huu utaletwa hapa Bungeni utakapokuwa tayari tumeshamaliza hayo mashauriano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hati ya Uhamisho wa Bajeti baina ya Mafungu, Na. 1 kwa Mwaka 2021/2022 *(Statement of Reallocation Between Votes – Reallocation Statement No. 1 of 2021/2022)*.

**11 NOVEMBA, 2022**

Hati ya Uhamisho wa Bajeti Ndani ya Mafungu Na.2  
kwa Mwaka 2021/2022 (*Statement of Reallocation within  
Votes – Reallocation Statement No. 2 of 2021/2022*).

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha  
na Mipango.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza  
na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Janeth Elias  
Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali  
lake.

Na. 139

**Mikopo kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuzungumza na taasisi za  
kifedha ili mikopo kwa watu wenye ulemavu itolewe kwa  
mtu mmoja mmoja badala ya vikundi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri  
Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA,  
VIJANA NA WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taasisi mbalimbali za kifedha ikiwemo mabanki zimekuwa zikitoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja na makundi mbalimbali wakiwemo watu wenye ulemavu. Aidha, wananchi wa kipato cha chini wakiwemo makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wanashindwa kunufaika na mikopo inayotolewa na taasisi hizo kutokana na mikopo hiyo kuambatana na vigezo vinavyowekwa ikiwemo waombaji kuwa na dhamana au mali isiyohamishika kama viwanja, mashamba na nyumba.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekuwa ikisimamia utoaji wa mikopo ya uwezesaji kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa mujibu wa kifungu 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019 na marekebisho yake ya mwaka 2021. Sheria na Kanuni hizi zimeelekeza kuwa mikopo hii itatolewa kwa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa uwiano wa asilimia nne kwa wanawake; nne kwa vijana na mbili kwa watu wenye walemavu kwa lengo la kuwawezesha kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za ujasiriamali ili kujiongezea kipato na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, habari njema ni kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya marekebisho ya

**11 NOVEMBA, 2022**

Kanuni mwaka 2021 ambayo yametoa fursa kwa mtu mmoja mmoja mwenye ulemavu kuomba mkopo. Hivyo, niombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba tufikishe taarifa hii ya mabadiliko ya kanuni za mikopo hiyo ambayo imetoa fursa kwa mtu mmoja mmoja mwenye Ulemavu kuomba mkopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. M AHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kufuatia majibu mazuri ya Serikali lakini bado changamoto inayoyakuta makundi haya ni pale unapokwenda kwenye taasisi za kifedha na kushindwa kufungua akaunti ya mtu mmoja. *(Makofi)*

Sasa ni lini Serikali itafanya makubaliano na mabenki ili makundi haya yaweze kunufaika na mikopo hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kufuatia hali ya watu wenye ulemavu na mazingira magumu ya biashara, je, Serikali haioni haja ya kuongezea muda marejesho makundi haya ikawa tofauti na makundi ya kinamama na vijana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janeth kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza naomba tulichukue kama ushauri na nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji huo kwamba tutaona namna bora ya kuwasaidi watu wetu katika kuona utaratibu wa kupata mikopo kupitia taasisi hizo kama alivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, la kuhusiana na muda wa marejesho ni kweli tumekwishakuliona hilo Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba watu wenye ulemavu ni kweli kwamba wanachangamoto. Unaweza ukakuta mtu wa kawaida ni tofauti na mtu mwenye ulemavu kwa sababu kuna wakati anahitaji kuwa na msaidizi ambaye yeye amekopa sawa, kama ni milioni 10 na mtu ambaye ni mzima naye ana milioni 10 lakini akienda kununua bidhaa atajikuta anahitaji kwenda na mtu wa kumsaidia kuona hizo bidhaa au kumsaidia kwenye usafiri.

Mheshimiwa Spika, pili hata atakapopata hitaji la chakula atahitaji amnunulie tena chakula msaidizi wake, na tatu hata anapokuwa anafanya biashara yake kwenye yale mazingira kama ni ana ulemavu wa kutokuona, atalazimika awe na mtu pale. Kwa hiyo, gharama inakuwa kubwa tofauti na hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeliona hilo na tunaona sasa namna gani ambavyo tunaweza tukaona utaratibu wa kubadilisha kanuni ili kuweza kuwanufaisha zaidi watu wenye ulemavu kwa sababu kama unavyofahamu hujafa hujauumbika sisi wote ni watarajiwa kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swali lake.

**11 NOVEMBA, 2022**

Na. 140

**Hitaji la Mwongozo wa Mishahara Sekta Binafsi**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa mwongozo wa upandishaji mishahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mishahara katika sekta binafsi unapanda baada ya Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara katika sekta binafsi ambayo inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 kufanya utafiti na kupanga viwango vya mishahara katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Bodi hiyo tayari imekamilisha kazi ya kupanga kima cha chini kipyaa na kumshauri Waziri mwenye dhamana na masuala ya kazi ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza kima cha chini cha mishahara kwa sekta binafsi. Kwa ujumla, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha suala hili na

**11 NOVEMBA, 2022**

itatangaza rasmi kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi mwezi huu wa Novemba, 2022. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa gharama za maisha kwa wananchi wote bila kujali kama wanafanya kazi sekta binafsi au sekta za umma ni zilezile gharama kama mchele, unga na gharama nyingine.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuhakikisha kwamba mishahara kwenye sekta binafsi na yenyewe inapanda inakuwa angalau shilingi 370,000 kama ilivyo kwa sekta ya umma? Kwa sababu sasa hivi maeneo mengi ni shilingi 100,000 kuendelea kidogo.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, amesema kwamba wanategemea kutoa mwongozo wa kupandisha mishahara kwa sekta binafsi mwezi Novemba; je, watakapotoa miongozo na mishahara itakapopanda, wakati wengine wa Serikali tayari wameshapandishiwa mishahara toka tarehe 1 Julai; je, mwongozo huo pia utalipa na malimbikizo kwa muda ambao wenzao wameshaanza kulipwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la nyongeza la Mbunge wa Arusha, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, kama ifuatavyo:-



**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza niseme tu kwamba katika mishahara hii ya watumishi wa umma na wale wa sekta binafsi kuna utofauti mkubwa. Katika sekta binafsi tunazo kada tofauti tofauti, wapo wafanyakazi wa mashambani, wapo wa viwandani, wapo ambao ni makampuni binafsi, wapo waliojijiri wenyewe na ambao wameweza kuajiri watu wachache. Kwa hiyo, uki-*standardize* na ukawa na *standard level* ya mishahara kwa kima cha chini inaweza ikaleta ugumu sana tumefanya *study* kuna *best practice* katika nchi nyingi ambazo tumeona kwamba huwezi uka-*standardize* kila mmoja na ndiyo maana bodi inaundwa ili ikafanye utafiti katika kuangalia uhalisia wa hali ya uchumi, lakini pia kazi zinazofanyika katika kila eneo ili iweze kuweza kupanga kulingana na *category* walizonazo hao wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wafanyakazi wa viwandani wana *category* yao, lakini pia na wale wa mashambani na maeneo mengine kulingana na uhalisia wa uchumi wa nchi husika. Kwa hiyo, tumelifanya hilo utafiti katika *best practice* ya nchi zaidi ya saba Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, niña imani kwamba bodi ya kima chini italeta ushauri ambao ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ndiyo mwenye dhamana ya kuamua kwamba hapo kuna haki? Kwa sababu tunachopaswa kuangalia ni zile kazi za staha lakini atumishi aweze kulipwa mishahara wake ambao unafanana na hali halisia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ameuliza kuhusu mishahara hii kwamba kwa upande wa Serikali tayari tumeshatangaza mabadiliko ya mishahara. Kwa upande wa *private sector* kama kutakuwa na malimbikizo.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa nchi yetu hatuna utaratibu wa *restrospectivity*, tuna utaratibu wa pale sheria au agizo linapotolewa ama kanuni, itakapopitishwa ndipo kwenda mbele hatua hiyo inafanyika. Kwa hiyo, hili suala la mishahara litaanzia pale kima cha chini kitakapokuwa kimerasimishwa na kutangazwa na Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Judith Kapinga.

Na. 141

**Hitaji la likizo ya uzazi kwa mwanamke anayejifungua mtoto njiti**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA K.n.y. MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini marekebisho ya sheria yataletwa Bungeni ili mwanamke anayejifungua mtoto njiti aongezewe likizo ya uzazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Na.183 kuhusu haki ya uzazi unaelekeza nchi wanachama kuweka utaratibu wa

## 11 NOVEMBA, 2022

kuwalinda mtoto na mama kutokana na changamoto za uzazi.

Mheshimiwa Spika, haki ya likizo ya uzazi kwa mwanamke mwajiriwa ipo kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura ya 366, Marejeo ya Mwaka 2019 kifungu cha 33 ambapo mwajiriwa mwanamke akijifungua mtoto mmoja anapewa likizo ya uzazi ya siku 84 na akijifungua watoto mapacha hupewa siku 100, kadhalika akijifungua mtoto njiti hupewa siku 84 katika mzunguko wake wa likizo.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa wafanyakazi wanawake wanapewa likizo ya uzazi kwa mujibu wa sheria na endapo likizo itamalizika na bado kuna uhitaji wa kumlea mtoto njiti, mwajiriwa anapaswa kujadiliana na mwajiri wake na kukubaliana kuhusu nyongeza ya likizo.

Vilevile mzazi anapokuwa amelazwa hospitalini na mtoto anapaswa kupewa *Exemption from Duty (ED)* ambayo itamwezesha mwajiriwa huyo kuendelea kulea mwanaye bila kupoteza haki ya kulipwa mshahara wake endapo atawasilisha cheti cha daktari kwa mwajiri wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria haijaainisha utaratibu mahususi wa kumwezesha mwanamke mwajiriwa kupewa likizo ya uzazi baada ya kujifungua mtoto njiti, ninapenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu imelipokea suala hili na italifanyia kazi kwa kufanya maboresho katika kanuni za sheria husika kuwawezesha waajiri kuandaa sera za ajira ambapo pamoja na mambo mengine suala la likizo kwa mwanamke atakayejifungua mtoto njiti litaanishwa kwa lengo la kumlinda mtoto njiti na mzazi wake. Ahsante.

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsanta, nashukuru kwa majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kutokana na upungufu wa vifaa vya makuzi kwa watoto njiti kwenye hospitali zetu; njia kubwa inayotumika kulelea watoto ni kwa kukubambatiwa na mama zao yaani *kangaroo style*.

Je, Serikali haioni kuchelewesha marekebisho ya sheria kunaendelea kuhatarisha afya na uhai wa watoto hao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, watoto njiti wana haki ya kuishi na kulelewa katika mazingira mazuri kama watoto wengine.

Je, Serikali haina *timeframe* ya kufanyia marekebisho ili kuhakikisha kwamba uhai wa watoto hao unalindwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Judith Kapinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imekwishakuanza kuchukua hatua mbalimbali za kufanya maboresho katika sekta ya afya ikiwemo pamoja na ununuzi wa vifaa ambavyo vinawasaidia watoto hawa kuweza kukua.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, lakini pili, katika eneo hilo hilo, maboresho yamekuwa yanafanyika na Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali ipo moja ya taasisi katika taasisi nyingi ambazo zinafanya na Serikali, *Doris Mollel Foundation* pamoja na Vodacom wamekuwa wakifanya kazi hii kwa kushirikiana na Serikali na maeneo mengi tumeona wamefanya kazi kubwa ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu haki ya watoto, tayari Serikali kwa kuona umuhimu wa watoto lakini pia *generation* tayari ilikwishatunga sheria ya mwaka 2009 sheria ya mtoto ambao inatoa haki, moja ya haki ya msingi ambayo iko kwenye Katiba, haki ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kufanya hivyo Serikali imeendelea kuboresha katika sekta ya afya na kuweza kuhakikisha kwamba katika mazingira haya hata mabadiliko ambayo yanatakiwa kufanyika kwa upande wa Serikali tunayachukua haraka sana na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu katika hatua ya awali, tulikwishakuwinda Dar es Salaam, na tukakutana na taasisi mbalimbali/Asasi za Kiraia ambazo zilikuwa na ajenda hii hii na nilikuwa mgeni rasmi katika shughuli hiyo ya kuweza kuona namna gani tunaweza tukachukua *best practice* katika nchi yetu kuweza kuona tunawasaidia mama hawa wanaojifungua watoto njiti na kupunguza vifo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**11 NOVEMBA, 2022**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa watoto njiti hao wana haki kabisa kama alivyosema mwenye kutujibia maswali kutoka Serikalini.

Ni kwa nini sasa basi Serikali hailipi gharama ya mtoto huyo wakati ambapo yuko hospitali na inalazimu wazazi kulipa mpaka milioni tano ikiwemo *Muhimbili Hospital?* (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maswali mazuri ya Mheshimiwa Katimba, lakini niseme kwanza moja kwa mwaka huu kwenye bajeti zimetengwa bajeti ya kujenga vituo vya watoto njiti 100, lakini katika *module* yetu ya kawaida pamoja kwamba hakuna sheria ambayo imetunga kwamba unampa mama huyu likizo, lakini kuna utaratibu wa ndani umekuwa ukifanyika wakati wote ambapo mama akitokea namna hiyo madaktari wanaandika na anapewa huduma.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye suala lako la kusema kwamba Serikali kwa nini hawalipii, kwenye mfuko wa bima kweli kulikuwa na changamoto hiyo kwamba anatokea mtoto njiti, lakini anatakiwa afanyiwe hivyo, lakini inaandikwa na sasa hivi tumeshaondoa hiyo na watoto njiti wanalipiwa na watoto chini ya miaka mitano huwa wanalipiwa bure kama sio bima. Kwenye mfuko wa bima ndio kulikuwa na shida na hiyo shida imeshamalizwa sasa hivi, watoto njiti wanahudumiwa kama kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, hao wanaolipa milioni tano ni wazazi wa aina gani? Maana Serikali

**11 NOVEMBA, 2022**

imeeleza nadhani umesikia majibu, hao wanaolipa shilingi milioni tano Muhimbili ni wazazi wapi?

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, mtoto njiti akizaliwa pale *Muhimbili Hospital*, anatakiwa alelewe mpaka afika ule umri ambao sasa mimba ingekuwa *term* na mtoto azaliwe na wengi wanakuwa na *complication*, lakini suala alilojibu Naibu Waziri mimi mwenyewe nilishafikisha kwake maombi ya kufadhili mtoto njiti ambaye alipitishwa kwangu na anaijua hiyo kesi ilifika mpaka shilingi milioni tano, ni watoto wa kawaida pamoja na hata wale waliokuwa kwenye *insurance* kama alivyoeleza yeye. Nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli alishanifikishia, mara nyingi kuna wenzetu kulikuwa na shida kweli Muhimbili, watoto wakipata matatizo si watoto tu hata wazee na watu wengine imekuwa kwamba wanakuwa-*charged* hasa hao watoto chini ya miaka mitano. Lakini tulipiga simu kwa sababu ni suala kisheria na halikuwa *exempted* na sasa tumeweka mfumo ambao hayo mambo hayajitokezi tena. Ahsante.

**SPIKA:** Sawa, tunafurahi kusikia kwamba hayo mambo hayajitokezi tena, hilo ni jibu la msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini sasa aulize swali lake.

**11 NOVEMBA, 2022**

Na. 142

**Barabara ya Magamba - Ifukutwa kuhamishiwa  
TANROADS**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, ni nini kinakwamisha barabara ya Magamba – Mtapenda - Kasokola hadi Ifukutwa kuhamishiwa TANROADS?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Magamba – Mtapenda - Kasokola hadi Ifukutwa ni mojawapo ya barabara iliyopendekezwa na Kikao cha Kumi na Nane cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Katavi kilichofanyika tarehe 23 Februari, 2022 kupandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Katavi kwa maana ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi alimwandikia barua Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi barua yenye Kumb. Na FA.364/423/01“C”/29 ya tarehe 11 Oktoba, 2022 kuomba kibali cha kupandishwa hadhi barabara za Wilaya ikiwemo barabara ya



**11 NOVEMBA, 2022**

Magamba – Mtapenda - Kasokola hadi Ifukutwa kuwa barabara za Mkoa. Mkoa utajulishwa na Waziri mwenye dhamana na barabara kupitia Gazeti la Serikali endapo imekidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kupitia **TARURA** tutaendelea kuihudumia barabara hii kwa kutenga fedha kwenye bajeti zetu ili iweze kupitika muda wote kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana pia nashukuru kwa majibu ya Serikali, ninalo swali moja tu la nyongeza.

Wakati Waziri mwenye dhamana akilisukuma jengo hili, je, Serikali haioni umuhimu wa kuigeuza barabara hii kuwa ya mzunguko au ya pete ili kuepusha Mji wa Mpanda na msongamano wa magari? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba hii barabara ni ya mzunguko kwa maana ya *ring road* ikiunganisha Halmashauri ya Nsimbo, Mpanda Manispaa pamoja na Halmashauri ya Tanganyika. Kwa hiyo, kwa umuhimu huo tunaitambua na ndiyo maana tunai-push zaidi ili iweze kupandishwa hadhi na iweze kuhudumia

**11 NOVEMBA, 2022**

watu wote kwa wakati wote. Kwa hiyo, jambo hilo Mheshimiwa Mbunge tumelipokea. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 143

### **Uhaba wa vipimo vya maabara Mtwara Vijijini**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza vipimo vya maabara hasa vya malaria katika zahanati za Mtwara Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Septemba, 2022, kipimo cha Malaria (*mRDT*), kuna vitepe vya kutosheleza matumizi ya miezi mitano na kabla ya kufika tarehe 30 Desemba, 2022 Bohari Kuu ya Dawa inategemea kupokea shehena nyingine ya vitendanishi hivyo vya malaria. Aidha, hali ya upatikanaji wa vitendanishi vya vipimo vya malaria katika Kanda ya Mtwara kufikia Oktoba, 2022 ni vitepe 631,825 ukilinganisha na matumizi ya vitepe hivyo ambavyo ni 84,150 kwa mwezi katika

**11 NOVEMBA, 2022**

Kanda ya Mtwara, hivyo kuna shehena ya kutosheleza miezi saba ijayo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuwakumbusha watumishi wanaohusika kuandaa taarifa na kuomba vitendanishi kwa ajili ya vipimo hivyo, kufanya maoteo kwa usahihi na kuomba kwa wakati maana vitendanishi hivyo vipo vya kutosha MSD Makao Makuu na kwenye Kanda husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa wataalam wa kusoma vipimo hivi; je, Serikali ina mpango gani wa kutuletea wataalam hao?

Swali langu la pili; je, Serikali haioni umuhimu wa kutusambazia vipimo vikubwa kwenye zahanati zetu pamoja na hospitali yetu ya Wilaya Nanguruwe ili tuweze kupima na magonjwa mengine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nimuondoe hofu, kadri Serikali itakavyoendelea kuajiri na kuongeza wataalam katika kada ya afya maana yake na mgawanyo huo utafika mpaka katika Jimbo lake la Mtwara Vijijini na maeneo mengine ya Taifa. Kwa hiyo, lipo katika mpango wa Serikali na tunaendelea kuajiri kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, umuhimu wa kuongeza vipimo vikubwa hilo lipo na ndiy kazi kubwa anayofanya Rais wa sasa Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Sasa hivi Ofisi ya Rais – TAMISEMI tukishirikiana na Wizara ya Afya, tunatarajia kupokea shilingi bilioni 169.7 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, vifaa tib ana vitendanishi kwa ajili ya maabara. Kwa hiyo tutaendeela kuvileta kwa kadri ambavyo vinapatikana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 144

**Changamoto ya usafiri Makao Makuu ya Jeshi la Polisi  
Mkoa wa Kaskazini Pemba**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya usafiri katika Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba?

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022 Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba umepatiwa magari matatu yaliyonunuliwa na Serikali ili kupunguza uhaba wa magari katika Mkoa huo. Serikali itaendelea kununua magari na pikipiki kila mwaka na kuzigawa katika Mikoa na Wilaya zenye uhitaji mkubwa ikiwemo Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, swali la nyongeza.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza na kwanza naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka kuuliza, je, kuna mkakati gani mahususi la kuongeza suala hili la usafiri katika Makao Makuu ya Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa sababu bado changamoto ni kubwa na hasa ukizingatia na vituo vidogo ambavyo vina mahitaji makubwa ya usafiri ikiwemo Kituo cha Mchangamdogo, lakini pia Kituo cha Mapana Kifuani ambacho nimekuzungumzia juzi? Ahsante sana.

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Asya Sharif Omar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, hivi sasa wamegaiwa magari matatu, tutaendelea kuwapatia magari ili wamudu kutekeleza majukumu ya ulinzi, usalama wa raia mali zao kadri tutakavyopata bajeti na kama anavyofahamu Mheshimiwa mwaka huu tumepitishiwa bajeti ya shilingi bilioni 15, yakanunuliwa magari, miongoni mwa maeneo yatakayopata magari ni pamoja na mikoa ya Pemba. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nimuulize swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar kuna polisi jamii, na polisi jamii hawa wanapelekwa kila Shehia katika Shehia za Zanzibar na shida yao kubwa ni mafuta.

Je, Serikali inatuambiaje kuwapatia walau mafuta, japo hawakupatiwa pikipiki lakini au maufuta yakuwafikisha katika vituo vyao vya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sio Zanzibar tu maeneo mbalimbali nchini Tanzania tunao utaratibu wa kuwa na polisi jamii kwa ajili ya kusaidia ulinzi shirikishi pale ambapo polisi wetu wanakuwa mbali na kwa sababu kama inavyoitwa polisi jamii uendeshaji wake kwa muda imekuwa ukichangiwa na wan jamii wenyewe. Sasa suala hili la kuzingatia kwenye upande wa mafuta ni suala kibajeti, tutalitafakari pale hali ya fedha na bajeti itakavyoruhusu tutaanza kuona uwezekano wa kuwafikiria mafuta na vyombo vya usafiri kama alivyotaja pikipiki. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Nyang'hwale ina vijiji 62 kata 15 na OCD wetu pale Wilayani ana gari moja na si zuri sana; je, Wizara ina mpango gani wa kutuongezea gari nyingine polisi Nyang'hwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema angalau yeye analo gari haliko vizuri sana lakini *at least* linatumika. Ushauri wetu gari hilo liendeleo kukarabatiwa, lakini kama nilivyokwishasema wakati namjibu Mheshimiwa Asya, tunao utaratibu wa kununua magari na kuyapeleka kule ambako yanahitaji sana.

Kwa hiyo, Nyang'hwale, kama sehemu ya Mkoa wa Geita tutauangalia kulingana na upatikanaji wa hayo magari ili waweze kupata gari linawezesha OCD wetu kufanya kazi yake vizuri. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. MBUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kishapu ina jumla ya kata 29 na ina vijiji 128 na Wilaya hii sasa haina gari hata moja, magari yote ni mabovu na kwa sasa hivi tumekuwa tukitumia gari moja ambayo tumeazimwa na Mgodini wa *Williamson Diamond Limited*.

Sasa Serikali inafanya jitihada gani za haraka kuhakikisha kwamba inapeleka angalau gari moja ya dharura kwa ajili ya kuokoa wananchi kupata huduma za msingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-



**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Kishapu inayochangamoto ya magari kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, gari walilonalo ni chakavu, linahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Nimpe matumaini Mheshimiwa Mbunge pale ambapo tutapata magari yanayotokana na bajeti hii tunayoitekeleza kipaumbele kitawekwa kule ambako hawana magari kabisa.

Kwa hiyo, kama Kishapu watakuwa hawana gari tutaelekeza *IGP* aipe Kishapu kipaumbele katika ugawaji wa magari hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, sasa aulize swali lake.

Na. 145

### **Kuweka ukomo wa upelelezi kwenye kesi za mauaji**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta muswada wa sheria wa kuweka ukomo wa upelelezi kwenye kesi za mauaji nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kesi za mauaji zinaangukia katika makosa makubwa (*capital offences*) zikiambatana na adhabu kubwa ambayo ni kunyongwa hadi kufa au kifungo cha maisha pale mtu anapopatikana na hatia. Hivyo upelelezi wake unahitaji muda na umakini mkubwa ndiyo maana kwa sasa upelelezi haujawekewa ukomo wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Mashtaka katika kuratibu na kusimamia upelelezi wa makosa ya jinai ametoa Mwongozo wa Mkurugenzi wa Mashtaka Na. 1 wa mwaka 2022 kuhusu ufunguaji wa mashtaka na ukamilishaji wa upelelezi wa kesi za jinai uliotolewa tarehe 30 Septemba, 2022 na kuanza kutumika tarehe 1 Oktoba, 2022. Mwongozo huo unataka upelelezi wa kesi za mauaji ambazo hazihitaji utaalum kutoka taasisi nyingine usichukue zaidi ya siku 60 na zile zinazohitaji utaalumu kutoka taasisi nyingine usichukue zaidi ya siku 90. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Katiba na Sheria na Naibu Waziri, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kupanua wigo wa haki za binadamu nchini Tanzania, nina swali moja la nyongeza.

**11 NOVEMBA, 2022**

Kwa kuwa mwongozo huu ni mwarobaini mzuri wa kusimamia haki za raia wetu nchini. Ni kwa nini mwongozo huu sasa usiingie kama sheria rasmi za nchi yetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi wazo lake tunalichukua na tutakwenda kulifanyia kazi kuona tuilete kama sheria au iendeleo kusimamia kwenye kanuni hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kwa niaba yake Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 146

### **Ujenzi wa barabara ya Singida hadi Kizaga Wilayani Ikungi**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Singida hadi Sepuka kuelekea Kizaga itajengwa kwa kiwango cha lami katika Wilaya ya Ikungi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago hadi Kizaga yenye urefu wa kilometa 77.6 na inategemea kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa...

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ....

**SPIKA:** Hujaitwa Mheshimiwa Kingu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

**SPIKA:** Ila ujue tu kwamba, haki yako ni swali moja. Kwa sababu swali unapewa la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Nilikuwa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali nyongeza kwamba kwa kuwa barabara hii ilitajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2015/2020

**11 NOVEMBA, 2022**

haikuteklezwa; ikatajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2020/2025 na mpaka sasa hivi tunavyozungumza bado hakuna mchakato wowote wa barabara hii.

Nini kauli ya Serikali kwa wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi na wananchi wa Mkoa wa Singida na Iramba kwa ujumla juu ya barabara hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi na kama alivyosema imetamkwa kwenye Ilani, Serikali inasema inategemea kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami mwishoni mwa mwezi huu wa kumi na mbili kwa ajili ya kuanza kujenga yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makambako - Songea tunajua kipande cha Songea mpaka mpaka na Njombe tayari kimeishapata mpango wake. Lakini kutoka mpakani mwa Songea na Njombe mpaka Makambako Serikali ina mkakati gani kuhusiana na kipande hiki cha barabara?

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na Uchukuzi, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kufanya matengenezo makubwa kwa barabara yote ya Makambako - Njombe hadi Songea. Kwa sasa kama alivyosema mpakani mwa Njombe na Ruvuma tayari tumeishapata fedha na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kufanya matengenezo makubwa kwa kipande ambacho kimeharibika sana kati ya Makambako - Njombe hadi mpakani mwa Mkoa wa Ruvuma, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Je, Serikali ina mpango gani wa barabara ya kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Simiyu kupitia Daraja la Sibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida na Mkoa wa Simiyu kupitia Daraja la Sibiti hivi ninavyoongea barabara zote tatu ziko kwenye kukamilisha usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami kuanzia Ulemo kwenda Sibiti, lakini pia kuanzia Iguguno kwenda Sibiti wakandarasi wako tayari wanafanya usanifu kwa ajili ya maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami kuunganisha hiyo mikoa miwili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Je ni lini barabara ya Karatu - Njia Panda kwenda Mang'ola - Matala hadi Lalago ambayo pia ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja kutoka Karatu - Mang'ola hadi Sibiti ni barabara kuu. Hata hivyo tumeisha kamilisha usanifu na Serikali inaendelea kutafuta fedha kujenga hiyo barabara ambayo inapita sehemu muhimu sana ya uchumi na hasa kilimo cha vitunguu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**11 NOVEMBA, 2022**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuiuliza Serikali; je, ni lini barabara yetu ya Bigwa - Kisaki ya kilometa 78 itaanza matengenezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taletale, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilitangazwa, lakini kilometa zilikuwa chache na sasa barabara hii tunategemea kuitangaza muda wowote kujenga kwa kiwango cha lami na tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi na barabara hii nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge itatangazwa mwaka huu wa fedha na itaanza kujengwa hizo kilometa 78, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona; barabara ya kutoka Kibena kwenda Madeke barabara hii ipo kwenye Ilani na Mheshimiwa Rais, juzi alisema barabara hii itajengwa kwa lami na Mbunge wa Lupembe amekuwa akizungumza mara kwa mara. Nini kauli ya Serikali juu ya barabara ya Kibena - Madeke? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona na Mbunge wa Lupembe umekaa naye hapo. Mheshimiwa Naibu, Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu



**11 NOVEMBA, 2022**

swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna maelekezo ambayo tumeyapata kwamba barabara hii ya Kibena *junction* - Madeke hadi Mlimba, Ifakara ijengwe kwa kiwango cha lami. Upande wa Morogoro ambako inakwenda tayari tumeshatangaza zabuni na upande wa Kibena kwenda Madeke ipo kwenye usanifu chini ya *African Development Bank*, lakini pia tunategemea tuanze kuijenga kwa kilometa chache kuanzia mwaka huu wa fedha, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 147

**Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Geita –  
Nyarugusu -Kahama**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, nini hatma ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Geita – Nyarugusu hadi Kahama hususani kipande cha Geita – Nyarugusu – Bulyanhulu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano ya msingi ya awali kati ya Serikali na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Barrick, Kampuni ya Barrick ilikubali kutoa dola za Kimarekani milioni 40 kugharamia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Hivyo, Serikali na Kampuni ya Barrick zimekubaliana kuwa fedha hizo kiasi cha dola za Kimarekani milioni 40 zitumike kwa ujenzi wa barabara ya Kahama – *Bulyanhulu junction* – Geita yenye kilometa 120 na kipande cha *Bulyanhulu junction* hadi Kakola (kilometa 11.3). Kwa sasa Serikali iko katika hatua ya kukamilisha majadiliano hayo ili kuwezesha mradi huo kuanza kutekelezwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya swali hili ambayo yanaonekana yanatia moyo kwamba kuna majadiliano. Lakini niombe Serikali majadiliano hayo yasichukue muda mrefu sana. Pamoja na majibu haya mazuri na swali moja la nyongeza.

Katika kuchochea uchumi shirikishi na shindani kuna barabara ndani ya Jimbo la Busanda kutoka Katoro kupita Kaseme kwenda Ushirombo, Jimboni Bukombe; je ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo ambayo imeishafanyiwa upembuzi yakinifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, barabara ya Katoro hadi Ushirombo imeishafanyiwa usanifu na sehemu ya barabara hii inatekelezwa na Mpango ama Mradi wa RAIS, lakini sehemu iliyobaki itaendelea kuhudumiwa na TANROADS na Serikali ina mpango wa kutafuta fedha kukamilisha barabara yote kipande kitakachobaki baada ya kile kipande kitakachojengwa na Mpango wa RAIS kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Mkomazi – Mnazi - *Umba junction* Maramba hadi Tanga iko katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukrasa wa 177 kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami; je, ni lini sasa mchakato wa kuanza upembuzi yakinifu utaanza katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja inayounganisha Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro iko kwenye Ilani na utekelezaji wa Ilani unaendelea. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunahakika kwamba tutaanza usanifu wa kina baada ya kufanya

**11 NOVEMBA, 2022**

upembuzi katika kipindi hiki cha miaka mitano katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwajengea Wananchi wa Jimbo la Nkenge Wilaya ya Misenyi barabara ya Mtukura kwenda Minziro na nikupongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe ulifika na barabara hiyo sasa imeamza kujengwa...

**SPIKA:** Swali.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** ...lakini ahadi ilikuwa ni ujenzi wa kiwango cha lami; je ni lini sasa barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kyombo, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilikuwa inafunguliwa na tumeishaifungua na baada ya kuifungua hatua inayofuata nikufanya upembuzi na usanifu na ndiyo tunavyoelekezwa na ilani kwamba barabara zote ziwe kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hiyo barabara itafanyiwa upembuzi na usanifu wa kina kadri fedha itakavyokuwa inapatikana, ahsante.

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kuhusu ujenzi wa barabara ya Morogoro - Njombe boarder Serikali imedhamiria kujenga kilometa 100 kwa maana ya *lot one* na *lot two*.

Swali naomba Serikali ithibitishie Wananchi wa Mrimba je, ni lini hizi kilometa 100 kwa *lot* zote hizi mbili zitaanza kujengwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunavyosema sasa hivi zabuni zimeishaandaliwa na tuko kwenye hatua za mwisho kutangaza hizo *lot* mbili ambayo ndiyo barabara inayokwenda kuunganisha na barabara ya Kibena - Madeke, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimwa Askofu Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASK. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipofika Bunju B, aliahidi kwamba barabara ya Bunju B kupitia Mabwepande itajengwa kwa kiwango cha lami; je,

**11 NOVEMBA, 2022**

unaweza kuwahakikishia wananchi wa Mabwepande kwamba itawekwa kwenye bajeti ijayo 2022/2023?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani bajeti ijayo ni 2023/2024; uliikusudia hiyo?

**MHE. ASK. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, naam.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwajima, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri na mimi nimeitembelea hii barabara na kama alivyoomba iwepo kwenye bajeti Bunge hili ndiyo litaamua hiyo barabara ipitishwe kuwa kwenye bajeti, lakini sisi kama Wizara tunategemea kuipendekeza iwepo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Agness Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante; ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami kipande cha barabara kutoka Masasi kwenda Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hokororo, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masasi - Nachingwea kilometa 45 imepangiwa bajeti kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, lakini pia kipande cha Masasi - Nachingwea hadi Liwale pia kimeingizwa kwenye Mpango wa EPC+F ambapo wakandarasi tayari wameishaoneshwa barabara hiyo na tayari tunategemea pengine kufungua zabuni kipindi si kirefu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mpango wa Serikali wa kujenga barabara ya *bypass* kuanzia Kata ya Kisasi - Unyamikumbi - Unyambwa mpaka Mtipa na *feasibility study* imeshafanyika; nataka kujua tu *commitment* ya Serikali ni lini ujenzi huu utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema usanifu umeishakamilika, sasa hivi Serikali inatafuta fedha ili

**11 NOVEMBA, 2022**

tuweze kuanza kujenga kipande hicho cha *bypass*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

Na.148

### **Sheria inayotumika kwenye Tozo za Bandari**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBEL** aliuliza:-

Je, ni sheria gani inayotumika kwenye tozo za bandari nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tozo za bandari zinatozwa kwa mujibu wa Sheria ya Bandari Namba 17 ya mwaka 2004. Kwa mujibu wa sheria hiyo, kitabu cha viwango vya tozo (*tariff book*) huidhinishwa na mdhibiti ambaye ni Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (*TASAC*).

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bandari Namba 17 ya mwaka 2004 imeeleza vyanzo vya mapato vya *TPA*



**11 NOVEMBA, 2022**

ambavyo vinajumuisha tozo za bandari (kifungu Na. 67). Aidha, sheria hiyo inaelekeza TPA kuandaa *tariff book* inayoainisha viwango vya tozo za bandari kwa kila huduma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE.OLIVER DANIEL SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Je Serikali haioni umuhimu wa kuwaelimisha watumiaji wa bandari ikiwemo ya Kemondo na Mwanza juu ya Sheria za Tozo zinazo zinazotungwa kuliko kukutana nazo barabani? (*Makofi*)

Swali langu la pili je, ni aina gani za tozo? Napenda kujua hilo, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoza tozo ama kutunga Sheria za Tozo kwanza unaanzishwa na Mamlaka ya Bandari yenyewe TPA na hatimaye unapelekwa kwa mdhibiti ambaye ndiye TASAC na TASAC ana wajibu wa kuitisha wadau wote wa sekta hiyo ama maeneo ambako hiyo tozo itakuwa inagusa katika tozo.

**11 NOVEMBA, 2022**

Sasa ninamuelekeza ambaye ndiye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari nchini pamoja na TASAC watoe elimu, waende katika hizi bandari za Kemondo pamoja na bandari zingine nchini kwenda kutoa elimu kwa jamii ili waeleze ni aina gani ya tozo wakienda bandarini watakutana nazo na kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili anataka Mheshimiwa Mbunge afahamu aina ya tozo ambazo bandari inatoza; tuna tozo ya aina nyingi, lakini zimegawanyika katika makundi mbalimbali; kuna tozo za lazima ambazo tunaita ni *ports statutory charges*, lakini kuna tozo tunazozita *wharfage*, *wharfage* ni aina ya tozo ambayo ukitumia miundombinu ya bandari unatozwa, lakini kuna tozo za *show handling* hizi ni tozo ambazo meli inapokuja mpaka kwenye gati la bandari inapokuwa inashusha mzigo ama kupakia mzigo pia unatoza na kuna tozo za ziada, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; ni lini Serikali itaweza kupitia upya tozo hizi ambazo zimekuwa nyingi bandarini na kuleta uwekezaji kutochochewa kuhusiana na hizi tozo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Bahati Ndingo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, tunauchukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na kimsingi tumeshaanza kukaa na wadau na mamlaka ambazo zinahusika kwa maana ya Tanzania ni TASAC, lakini kwa wenzetu Zanzibar ni ZMA ambako zina mahusiano ya moja kwa moja na vikao hivyo vinaendelea, na wewe Mheshimiwa Mbunge ukipata nafasi tutakukaribisha kama mdau ili utoe maoni ya Waheshimiwa wengine, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 149

### **Hitaji la vifaa kingaradi, Mwese, Katavi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa kingaradi katika eneo la Mwese lenye milipuko ya radi mara kwa mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

## 11 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kuna maeneo yenye matukio mengi na makubwa ya radi hususan eneo la Mwese Mkoani Katavi. Hali hii husababisha nguzo nyingi za umeme, transfoma na vifaa vingine vya umeme kuharibiwa na radi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022 Serikali imetenga shilingi milioni 502 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya umeme katika Mkoa wa Katavi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa nguzo za zege, transfoma zenye kuhimili madhara ya radi (*surge arresters*) na kuweka waya (*overhead shield wire*) katika maeneo yenye matukio ya milipuko ya radi mara kwa mara ikiwemo kingaradi eneo la Mwese, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, swali langu la msingi nimeomba kupatiwa vifaa kingaradi kwenye eneo la Mwese.

Je, Serikali ni lini itapeleka hivyo vifaa kwa kuwa, eneo hilo lina radi za mara kwa mara na wananchi wengi wamekuwa wakipoteza maisha yao na mali zao, hasa mifugo?

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya msingi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze vifaa hivyo vitafika lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 bado unaendelea na sasa tuko katika robo ya pili, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha hii pesa imeenda na kwenye maeneo hayo ya Mwese pia, vifaa hivi vitafika kwa kukamilisha na hiyo miundombinu ya umeme ambayo inahitajika katika maeneo hayo kwa haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, haya majibu ya swali la msingi hayajajibu swali la Mheshimiwa Mbunge. Mbunge anauliza, anataka vifaa ili wananchi wake na mifugo ikingwe dhidi ya radi. Wizara inaeleza upande wake kwamba ninyi mtakhakikisha miundombinu ya umeme inayoharibiwa mtakuwa mkiitengeneza, kwa hiyo, kidogo swali lake yeye anataka vifaa vinavyozuia radi na wewe si unajua kule ndio radi ziko nyingi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, msaidieni Mheshimiwa Mbunge, vifo ni vingi huko kutokana na radi, ndio hoja yake. Anataka vifaa vinavyokinga radi, hili la umeme ni lingine, sasa sijajua kama hii radi ni ninyi ndio mnatoa hivyo vifaa ama ni nani yuko Serikalini, lakini hoja ya Mheshimiwa Mbunge anataka vifaa vinavyokinga radi, ili mifugo, wananchi na mimea iweze kuwa salama.

Sawa, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**11 NOVEMBA, 2022**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther Midimu.

Na. 150

### **Hitaji la Chuo cha VETA, Busega**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU K.n.y. MHE. MINZA S. MJIKA**  
aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilayani Busega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, majibu

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya VETA katika Wilaya 63 ambazo hazina vyuo hivyo, kiasi hiki pia kitatumika katika ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, Busega ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa vyuo

**11 NOVEMBA, 2022**

vya ufundi stadi katika mwaka huu wa fedha. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa pesa za ujenzi wa VETA ya Mkoa wa Simiyu na mpaka sasa ujenzi unaendelea. Kwa kuwa sSera ya Serikali ni ujenzi wa VETA kila Wilaya; ni lini sasa Serikali itajenga VETA katika Wilaya ya Simiyu ambayo haina VETA?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kujenga vyuo hivi katika Wilaya ambazo hazina vyuo na hivi sasa tuko katika mkakati au mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa VETA hizi. Mara tu pesa zitakapopatikana tutahakikisha kwamba, tunaanza ujenzi mara moja. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rorya ni moja ya Wilaya ambazo na sisi tumeanza mchakato wa muda mrefu sana kwa ajili ya maombi ya kupata Chuo cha VETA, na Mheshimiwa Waziri unakumbuka nimekuwa nikikusumbua sana kwa muda mrefu ili angalau na sisi tuweze kupata chuo cha VETA. Nilitaka nijue sasa kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu katika vyo vya VETA 63 kama na sisi Wilaya ya Rorya tumo katika vyo hivyo?  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sijajua kama ile orodha unayo kichwani, ili ukumbuke Rorya kama imo. Kama hukumbuki unaweza ukamjibu Mheshimiwa Mbunge baada ya kuipitia hiyo orodha ama kama unaikumbuka hiyo Wilaya unaweza kumpatia majibu sasa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya zilizobaki ambazo hazina Vyo vya VETA ni Wilaya 63, tafsiri yake Wilaya ya Rorya nayo imo katika ile orodha. Tafsiri yake tunataka tujenge katika Wilaya zote ambazo hazina vyo kwa awamu. Kwa hiyo, katika awamu ya kwanza tutaanza kwa Wilaya zote ambazo hazina kwa pamoja katika mwaka huu wa fedha na mwaka unaofuata ina maana tutakuwa na jukumu la kumaliza kazi ile ambayo tutakuwa tumeianza katika mwaka huu wa fedha. Nakushukuru sana.



**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Singida imeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa VETA na uhitaji ni mkubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini kwa ajili ya chuo hiki.

Naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri; je, Halmashauri ya Wilaya ya Singida nayo imo katika kupata chuo hiki? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhani, Mbunge wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Singida ninachofahamu kuna Chuo cha VETA cha Mkoa wa Singida ambacho kipo katika Wilaya ya Singida. Kwa hiyo, maadam tuna chuo cha VETA cha Mkoa ambacho kipo katika Wilaya ya Singida, hatuwezi tena kwenda kujenga chuo kingine katika Wilaya hiyo hiyo. Kwa hiyo, kile Chuo cha VETA cha Mkoa wa Singida ndicho ambacho kitatumika kama chuo cha Wilaya ya Singida. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

**11 NOVEMBA, 2022**

Na. 151

**Ujenzi wa Chuo cha VETA, Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilayani Tunduru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya VETA katika Wilaya 63 ambazo hazina vyuo hivyo, kiasi hiki pia kitatumika katika ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, Tunduru ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa vyuo vya ufundi stadi katika mwaka huu wa fedha. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**11 NOVEMBA, 2022**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuwa na azma nzuri ya ujenzi wa Vyuo vya VETA katika Wilaya zote 63. Swali dogo tu la nyongeza, je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa vyuo hivyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza kueleza katika swali la mwanzo kwamba vyuo hivi tutajenga vyote kwa pamoja na tunachosubiri sasa ni upatikanaji wa fedha ambazo ndizo tumeshafanya maombi kwa Wizara ya Fedha na Mipango; na mara tu tutakapopata fedha hizi ujenzi huu utaanza kwenye vyuo vyote 63 katika Wilaya zote 63 kwa pamoja. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante; katika hesabu ya Halmashauri 63, je, na Mbogwe imo kwenye hesabu hiyo Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemus Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mbogwe ni Wilaya, sina uhakika sana kwa sababu kuna Wilaya ambazo zina majimbo mawili. Kwa hiyo, hapa kwenye majimbo mawili ina maana tunapokwenda kujenga ni Wilayani, sasa kama Mbogwe ni Wilaya ambayo inajitegemea itakuwa imo, lakini kama Mbogwe ni jimbo miongoni mwa Wilaya ina maana tutakapokwenda kujenga ni Wilayani ambako na Mbogwe ita-*share* chuo hicho ambacho kitajengwa katika Wilaya hiyo ambayo Mbogwe ipo kwenye Wilaya husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, Mbogwe ni Wilaya ni Jimbo?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, Mbogwe ni Wilaya pia ni jimbo inajitegemea. Kwa hiyo, nilitaka kujua tu kama itajengewa chuo mwaka huu.

**SPIKA:** Haya, basi Mheshimiwa Waziri hilo ameshajibu. Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, kwanza naomba niishukuru Serikali kwa kujenga Chuo cha VETA pale Uvinza.

Sasa nauliza; ni lini chuo kile kitafanya kazi ili watoto wa pale waweze kuanza kuingia chuoni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Nashon, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna vyuo vyetu 25 vya Wilaya ambavyo tulianza ujenzi wake toka mwaka 2021 na ujenzi ule uko kwenye hatua za mwisho. Hivi sasa tunatengeneza samani au tunasambaza samani pamoja na vifaa vya kufundishia. Ni matarajio yetu katika mwaka ujao, 2023 vyuo hivi 25 vya Wilaya pamoja na vile vinne vya mikoa vitaanza kutoa mafunzo rasmi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi; elimu ya ufundi ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote.

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muhimu kubadilisha utaratibu, badala ya kujenga hivi vyuo kiwilaya ijenge kijimbo kwa sababu, kuna Wilaya nyingine ambazo zina majimbo mawili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kada hii ya ufundi ni muhimu, naomba tuchukue ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, hivi sasa tumeanza katika ngazi ya kanda,

**11 NOVEMBA, 2022**

mikoa pamoja na ngazi ya Wilaya. Tuangalie baadaye namna gani tunaweza tukafika katika ngazi ya jimbo kama Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri.

Kwa hiyo, tunaubeba ushauri wako tunakwenda kuufanyia kazi na tufanye tathmini ya kina. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 152

**Mkakati wa kuiwezesha GST kufanya utafiti kuhusu *Critical Minerals***

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kuiwezesha GST kufanya utafiti wa kisayansi na teknolojia kuhusu *Critical Minerals* ili kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini imeielekeza Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*) kuandaa taarifa kuhusiana na madini mkakati (*Strategic/Critical Minerals*) hasa madini teknolojia ikiwemo madini muhimu kwa ajili ya nishati ya kijani (*green energy minerals*). *GST* imeanza kuandaa andiko kuhusiana na madini haya na kuainisha ni madini yapi ndiyo ya kimkakati kwa mtizamo wa dunia na nchi, matumizi ya madini hayo na mahala yanapopatikana.

Aidha, *GST* imebaini maeneo ya kufanya tafiti za jiofizikia katika maeneo sita (*blocks*) kwa nishati ya kijani (*green energy*) na matumizi ya magari ya umeme. Serikali inaendelea kutafuta wadau wa maendeleo ambao watashirikiana katika kufanya tafiti za jiosayansi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali kuhusiana na utayari wao kwenye suala la madini muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumeona thamani ya fedha kwenye ongezeko la asilimia 9.4 kwenye bajeti ya *GST* mwaka wa fedha huu unaoendelea ambapo mapato yame-*shoot* mpaka asilimia 141.

Ni kwa nini sasa Serikali isilete mkakati wa dharura kwa ajili ya ku-*fund* *GST* ili iweze kufanya tafiti za kisayansi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili; sasa hivi tunapozungumza *GST* imefikia wapi na Serikali imefikia wapi kwenye masuala ya *critical minerals* kwenye utafiti na uchimbaji? (*Makofi*)

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza; ili kuboresha teknolojia ya kutafuta madini na hasa tafiti ya madini haya ya kisasa, GST kupitia Wizara yetu ya Madini imeanza mkakati rasmi wa kuanzisha mashirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na nje na kuandika maandiko mahsusi ambayo yatatusaidia kupata fedha za kuwekeza katika utafiti wa madini ya kimkakati. Tuna Kampuni ya *Noble Helium* ambayo inashirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na GST, tuna Kampuni ya *Rocket Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kuhusu hatua ambazo tumeshafikia katika kutafiti na kuzalisha madini ya kimkakati; ni kwamba sisi kupitia Tume yetu ya Madini kama Wizara, tayari tunatoa leseni za utafiti wa madini ya kimkakati kwa ajili ya utafutaji wa madini na uchimbaji wa madini. Na Serikali imekuwa na ubia na baadhi ya kampuni hizo na kwa ruhusa yako naomba nitaje chache.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Lindi, tuna kampuni inayoitwa *Lindi Jumbo Limited* wenye leseni ya uchimbaji wa kati na wanaendelea na utafiti na sasa hivi wamefikia hatua ya kuendeleza ujenzi wa eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo Mkoani Lindi tuna Kampuni inaitwa *Ngwena Tanzania Limited*, wana leseni



**11 NOVEMBA, 2022**

za utafiti wa madini ya kinywe na sasa hivi wako katika hatua ya uthamini kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Na pia wale wa Jumbo nao wanafanya utafiti wa madini ya kinywe.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Morogoro tuna...

**SPIKA:** Kampuni zimetosha Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hizi chache nipende tu kumhakikishia kwamba sasa hivi Tanzania imeamka na wawekezaji wakubwa wa ndani na nje wanajihusisha na utafutaji wa madini ya kimkakati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo.

Na. 153

**Kuboresha mawasiliano ya simu Kata za  
Makurunge na Fukayosi**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO K.n.y. MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha minara ya mawasiliano ya simu katika Kata za Makurunge na Fukayosi?

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imezijumuisha Kata za Makurunge na Fukayosi katika Mradi wa Tanzania ya Kidigitali unaotekelezwa kwa fedha kutoka Benki ya Dunia ambapo zabuni ya mradi huo imeshatangazwa tarehe 24 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kata hizo zitapata huduma za mawasiliano kwa teknolojia za 2G, 3G na 4G. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini nitumie nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali, nimepitia taarifa yao ya miradi ya Tanzania ya Kidigitali, nimeona Kata za Gwata, Bokomnemela na Dutumi zimewekwa kwenye orodha ya Kata 763; nawashukuru sana Serikali. *(Makofi)*

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, sasa swali la nyongeza; je, ni lini wakandarasi hawa ambao wameshapatikana watafika kwenye kata hizo na kuanza utekelezaji wa mradi husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kwa kiwango gani huduma ya 3G inawasaidia Watanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tender hii ilitangazwa tarehe 24...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, huyo aliyauliza ameuliza kwa niaba, yeye anaitwa Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini. Ameuliza swali la msingi kwa niaba, lakini maswali ya nyongeza yeye ndio ameuliza.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha kwa niaba ya Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo: -

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumejibu katika swali la msingi, *tender* ya upatikanaji wa mawasiliano katika miradi ya *World Bank* ambayo ilitangazwa tarehe 24 itafunguliwa tarehe 2 Desemba. Na baada ya kufunguliwa, mchakato wa upatikanaji wa vibali na hatimaye kuanza kwa hatua za ujenzi utakapokamilika ujenzi wa mawasiliano katika hizo kata utaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika kipande cha pili cha swali la Mheshimiwa Mwakamo, ni kwamba huduma ya 3G itawafikia lini Watanzania?

Mheshimiwa Spika, labda nitoe tu takwimu za harakaharaka; katika teknolojia ya 2G mpaka sasa kwa *population coverage* mpaka sasa Tanzania tumefikia asilimia 96; lakini kwa 3G tumeshafikia asilimia 72; 4G tumeshafikia asilimia 55. *Internet penetration* mpaka sasa kwa nchi yetu ni asilimia 50. ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ya swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika orodha aliyotoa Mheshimiwa Waziri ya usambazaji wa minara vijijini kata zangu za Kaengesa, Mfinga, Izimba na Milepa hazimo; je, Serikali mna mpango gani wa kupeleka minara katika kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo uliagiza Wizara yetu tulete orodha hapa Bungeni, orodha hiyo ina *segments* mbalimbali; ina *borders and special zone, phase six*, miradi 763, vijiji ambavyo vimeshafanyiwa tathmini 2,116. Kama ukiangalia kwenye kata 763 haupo, basi tunaamini kabisa katika vijiji 2,116 unaweza ukawemo. Na kama utakuwa haupo basi tunaamini kwamba katika hatua za kuendelea kufanya tathmini tutaviingiza vijiji hivyo ili vipate mawasiliano, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi.

Na. 154

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji – Mufindi**

**MHE. NANCY H. NYALUSI K.n.y. MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

**11 NOVEMBA, 2022**

Je, lini skimu za umwagiliaji Ukanda wa joto lhowanza, Malangali, Idunda, Mbalamaziwa, Itandulu, Nyololo na Maduma zitajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika Mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 itatenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za Ukanda wa joto za lhowanza, Malagali Idunda, Mbalamaziwa, Itandu, Nyololo na Maduma. Baada ya kukamilisha zoezi hili Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa skimu hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, skimu ya umwagiliaji ya Mgololo ambayo ina hekta 700 ilijengwa na Serikali kwa shilingi bilioni 1.9 ambayo ilikamilika mwaka 2012, mwaka 2013 ikaanza kutumika na mwaka 2013 hiyo hiyo mifereji ikaanza kuvujisha maji kwa sababu ilikuwa ni mibovu.

**11 NOVEMBA, 2022**

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza kujenga mifereji hiyo ili kuokoa pesa yake iliyotolewa, lakini pia kwa sababu mradi huo haujakamilika na haujawanufaisha wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nancy Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Skimu hii ya Mgololo ni muhimu kwa sababu inahusisha Kata mbili za Makungu na Kiyowela na humo ndani kuna vijiji zaidi ya tisa ambavyo vinanufaika na mradi huu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti yetu inayokuja tutauingiza mradi huu kwa ajili ya utekelezaji ili kuweza kurekebisha mapungufu yote na uweze kuwanufaisha wananchi, hasa wa Vijiji vya Lugolofu, Kitasengwa, Lugema, Mabaoni, Makungu na Lole.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi; je, Serikali itajenga lini skimu ya umwagiliaji katika Bonde la Eyasi ili kuboresha kilimo cha umwagiliaji unaoendelea kwenye bonde hilo?

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha Skimu za Eyasi zimebainishwa kuwa ni sehemu ya utekelezaji katika bajeti hii na katika utekelezaji wa mradi huo hivi sasa tupo katika hatua ya manunuzi ya kumpata mkandarasi ili utekelezaji uanze mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpebenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni nini mkakati wa Serikali wa kuwasaidia wananchi na wawekezaji katika Kata ya Mtunda kwenye Jimbo la Kibiti katika miundombinu ya umwagiliaji ukizingatia kwamba kuna uwekezaji mkubwa sana wa kilimo cha mpunga umefanyika pale na unaendelea wa ekari zisizopungua 20,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Twaha Mpebenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo: -



**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekuwa tukisema hapa tunatambua kwamba Bonde la Rufiji ni kati ya mabonde muhimu katika kilimo cha umwagiliaji hapa nchini Tanzania na ndiyo maana katika mkakati wetu wa mwaka huu katika bajeti yetu, tumeamua kuyapitia mabonde yote 22 likiwemo Bonde la Rufiji kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili baadaye tuje tutekeleze miradi mikubwa ya umwagiliaji ambayo pia itawagusa wananchi wa Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Kongogo ni moja ya skimu ambazo ziliwekwa kwenye bajeti ya 2022/2023; je, Serikali imefikia wapi katika kuanza utekelezaji wa ujenzi wa skimu hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo: -

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, ni kweli Skimu ya Kongogo ipo katika bajeti ya mwaka huu na hatua ambayo tumeifikia, mkandarasi ameshapatikana na muda wowote kuanzia hivi sasa atakwenda kuanza utekelezaji wa ujenzi wa skimu hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Arusha Chini iliyopo Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ni miongoni mwa skimu ambazo zitafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu kwa mwaka huu wa fedha; je, ni lini kazi hiyo itaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli skimu hii ilibainishwa na kuwekwa katika mpango wetu wa utekelezaji katika mwaka huu wa fedha. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kufanya kazi ya kukamilisha taratibu zote kwa ajili ya manunuzi na hatua nyinginezo ili kazi hizi zianze kwa uharaka.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kufikia Disemba mwaka huu tutakuwa tumefika hatua kubwa sana katika miradi yote, na hivyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi hiki cha muda mfupi, eneo lake hilo pia litajumuishwa na tutaanza kazi hiyo ya usanifu na upembuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwenye Mradi wa *Songwe River Basin* kuna *package* inayounganisha eneo la umwagiliaji la hekta zaidi ya 3,500 pale Kyela.

Je, Serikali imefikia wapi kuungana na Malawi kuanza kutekeleza mradi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema muuliza swali, Mheshimiwa Mbunge, amelitaja Bonde la Mto Songwe ambalo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huu. Kazi ambayo Wizara inafanya hivi sasa ni kuhakikisha tunaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu wa haya mambonde yote, lengo letu kubwa ni kuwa na miradi

**11 NOVEMBA, 2022**

mikubwa ambayo itahusisha miradi ambayo pia Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mwaka huu wa fedha tayari tumeshawapa kazi washauri elekezi kwa ajili ya kuanza kazi hii na tunategemea kwamba mabonde yote yale 22 kuanzia Bonde la Ziwa Victoria, Malagarasi, Manonga, Wembele, Bonde la Ruvuma, Bonde la Rufiji, Bonde la Mto Songwe, Ifakara Idete, Kilombero, Mkomazi, haya yote yapo katika mpango na yatakwenda kukata kiu ya wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona bado mmesimama na Waziri kashataja skimu zenu zote. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nafurahi sana.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaniambia ni lini ukarabati wa skimu zilizo kwenye Kata ya Kahe Magharibi na mifereji iliyo kwenye Kata za Marangu Mashariki, Kirua Vunjo na Kilema utafanyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, tuna orodha ya miradi mingi sana ambayo mwaka huu wa fedha tunaifanyia kazi. Hivyo, nitaomba mimi na Mheshimiwa Mbunge tukae tuangalie maeneo ambayo tutayafanyia utekelezaji mwaka huu katika Mkoa wa Kilimanjaro ni yapi, na ya mwaka unaokuja ni yapi, ili kama hayapo katika mwaka huu wa fedha basi tuyaingize kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha. Lakini lengo letu ni kuhakikisha mifereji yote hii inafanyiwa kazi na wakulima wa kutoka Jimboni kwa Mheshimiwa Kimei wanapata fursa ya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Kidoka ni kati ya skimu zilizopo kwenye Mkoa wa Dodoma, lakini skimu ile miundombinu yake imekuwa chakavu na wakulima wetu wamekuwa wakijiendesha kwa hasara sana kutokana na gharama kubwa za umeme wanazozitumia ku-pump maji.

**SPIKA:** Swali?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Je, ni lini sasa Serikali mtakwenda kuweka miundombinu rafiki ya skimu ile ili wananchi wetu waweze kujiendesha vizuri kwa faida? Ahsante.

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja kati ya kazi kubwa ambazo tuliwapa watu wa tume ni kuhakikisha wana-*take stock* ya miradi yote ambayo imekwama na yenye changamoto, na tumekamilisha zoezi hilo. Hivi sasa ni kuanza kupitia na kuona namna gani tunaweza tukaboresha skimu hizo.

Mheshimiwa Spika, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitatoa maelekezo kwa watu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuhakikisha Jumatatu wawepo katika eneo la Kidoka kuangalia changamoto ni ipi na tuone namna ya kuweza kurekebisha skimu hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali fupi.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kalenga lina skimu 19 na nyingi ni chakavu; je, ni lini sasa Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya ukarabati huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali la Mheshimiwa Kunti, tunayo stock ya miradi yote ambayo ina changamoto na nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaingiza miradi yake pia katika mpango wetu na tutaipitia kuona inahitaji marekebisho gani.

Mheshimiwa Spika, lakini lengo letu kubwa hasa; sisi tulifanya kazi ya kupitia miradi yote, tunataka tufanye kilimo cha umwagiliaji kwa hiyo hatutaliacha eneo lolote, tutayafikia maeneo yote. Lengo letu ni kwenda katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Wakulima wa skimu za umwagiliaji Matebete, Chosi, Herman, Isenyela wanapata shida sana wakati wa uhaba wa mvua kwa kupeana zamu usiku, na wengi wao wanazunguka na mapanga usiku kucha.

**SPIKA:** Swali?

**11 NOVEMBA, 2022**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Je, Serikali itawaboreshea skimu hizi lini ili kuondoa adha hii na waweze kulima kwa tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mbarali tuna miradi ya umwagiliaji ambayo tumeitengea fedha ya kiasi cha shilingi bilioni 61 ambayo inahusisha Herman Chosi, Bonokuva Gigolo na kwenda katika Matebete, tunakwenda Ifenyela na Uturo. Haya yote niliyoyataja wakandarasi wameshapatikana na muda wowote kazi ya utekelezaji wa miradi hii unanza.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 155

### **Kuimarisha Huduma za Afya Nchini**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-



**11 NOVEMBA, 2022**

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma za afya zikiwemo dawa muhimu katika hospitali zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya nchini kwa kuboresha miundombinu ikiwemo kuweka vifaa tiba vya kisasa, kuajiri wataalam wa afya pamoja na kuwapandisha madaraja ili kuongeza morali ya kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni 200 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba na hadi kufikia tarehe 30 Oktoba, 2022, Serikali imekwisha toa jumla ya shilingi bilioni 74.3 kwa ajili ya manunuzi ya dawa na vifaa tiba ili kuimarisha upatikanaji wake katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete swali la nyongeza.

**11 NOVEMBA, 2022**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa nakushukuru sana lakini pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya vifaa tiba ikiwemo vitanda vya kujifungulia akina mama katika Mkoa wa Mara.

Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi na akina mama wa Mkoa wa Mara kwamba endapo italetwa vifaa tiba hivyo hospitali pamoja na Vituo vya Afya vya Mkoa wa Mara vitapata vitanda kwa ajili ya kuondoa tatizo hilo?

Swali la pili; je, Serikali imejipanga vipi kuthibiti wizi wa dawa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu siyo mara ya kwanza kufika Wizarani akizungumzia Hospitali yake ya Mkoa wa Mara. Lakini nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa sababu yeye anajua kwa sasa tayari vifaa vyenye thamani ya bilioni tatu zimeshapelekwa Mkoa wa Mara na hapa tunapongea tayari *CT Scan* ipo pale Mkoani Mara na *Digital Xray* inangojea tu jengo liishe ili kazi ianze.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kuwa hospitali ya Mkoa wa Mara tumeshakubaliana ndani ya Wizaru na Waziri wa Afya ameshatoa maelekezo tarehe 12 na Mkoa wamekubaliana na maelekezo ya tarehe 12 Disemba hospitali hiyo inaenda kuanza na watumishi watahama

**11 NOVEMBA, 2022**

kwenye hospitali waliyokuwepo ili wahamie kwenye hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili la suala kuwa tumejipangaje kudhibiti wizi wa dawa. Moja, tumetengeneza mfumo ambao MSD sasa wataweza ku-track dawa kuanzia zinapotoka Taifani mpaka zinapofika kituoni. Wakati huo huo kama Wabunge mnakumbuka tulikuja hapa kwenu na kuwaonesha mianya ambayo inapotea dawa zinapofika kwenye Wilaya zetu na Mikoa yetu. Ushirikishwaji huo sio kwamba tulikuwa tunasema wizi wa dawa, lakini tulitaka kumleta kila mtu *on board* tujue wote ili tuweze kushirikiana kusimamia na sasa kule kwenye zahanati zetu, vituo vyetu vya afya, hospitali zetu za Wilaya tunashirikisha jamii na Waziri wa Afya ameshatoa maelekezo kwamba dawa ikitoka MSD inapofika Wilayani, Mkuu wa Wilaya ajue, Mkurugenzi ajue, lakini Mbunge apewe copy ili wote pamoja na zile Kamati za Afya za zahanati, za vituo vya afya na Wilaya wajue dawa iliyoingia ili kwa pamoja tushirikiane kulinda huu ubadhirifu ambao umekuwa ukitokea kwenye nchi yetu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa pale Musoma Mjini hatuna Hospitali ya Wilaya na nimekuwa nikiomba mara nyingi Serikali iweze kutukabidhi ile hospitali iliyopo ambayo ni ya Mkoa na imeahidi kwa muda mrefu.

**11 NOVEMBA, 2022**

Napenda kujua ni lini sasa rasmi Serikali itatukabidhi ile hospitali iwe Hospitali ya Manispaa ya Musoma ili huduma bora zaidi ziweze kupatikana kwa watu wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nimesema ni tarehe 12 Disemba, 2022 wanaanza kuhama kwenda kwenye hospitali mpya halafu mnakabidhiwa Hospitali ya Wilaya na ibaki kutumika namna hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ya Kitete bado ina upungufu mkubwa wa dawa, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inapunguza tatizo hilo la upungufu wa dawa katika Hospitali ya Kitete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa asilimia na kwa rekodi ambazo zimetoka MSD kwa sasa upatikanaji wa dawa ni asilimia 78 maana yake tuna upungufu wa asilimia 22. Moja ya namna ya kufanya ni kuchukua mapato ya ndani ambayo Hospitali ya Kitete inapata itumie kununua dawa palepale Tabora kama hazitakuwepo pale MSD.

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Hospitali ya Kanda ya Mtwara bado inaupungufu mkubwa katika kuikamilisha kiujenzi, lakini pia vifaa tiba. Lakini Kanda yote ya Kusini inaitegemea hospitali hiyo kwa muda mrefu.

Sasa ni lini hospitali hiyo itakamilika ili kuwaondolea adha wananchi wa Kusini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba kwa kweli Hospitali ile ya Kanda ya Mtwara ni mojawapo ya hospitali nchini ambayo imejengwa kwa majengo ya kisasa mno. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kazi kubwa ambayo imefanyika pale, mwaka huu wametengewa shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuendelea na ujenzi ili kukamilisha mambo ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema hayajakamilika. Niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa namna anavyofatilia shughuli za Mkoa wake.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema sasa aulize swali lake.

**11 NOVEMBA, 2022**

Na. 156

**Kuwavuna tumbili katika Kisiwa cha Juma-Sengerema**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawavuna tumbili katika Kisiwa cha Juma Wilayani Sengerema ambao wanakula mazao ya wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Jimbo la Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi ya kuyabaini na kuyadhibiti makundi (familia) ya tumbili yanayosumbua wananchi katika Kisiwa cha Juma, Wilayani Sengerema. Aidha, Serikali itaendelea kuhamisha makundi hayo na kuyapeleka katika hifadhi nyingine zenye mahitaji ya wanyamapori hao. Wizara itaendelea kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapori waharibifu wakiwemo tumbili na nyani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam umekaa na nawakumbusha kila siku ni lazima usimame. Ningemwita Mbunge mwingine hapo. Mheshimiwa Tabasam swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuwa tayari kuhamisha makundi hayo

**11 NOVEMBA, 2022**

ya tumbili hao katika Kisiwa cha Juma, lakini bado kuna tatizo la mamba katika mialo yetu hasa mwalo wa Buyagu, Irunda pamoja na Rugongo.

Je, Serikali ipo tayari kutujengea vizimba kwa ajili ya kuondoa huo usumbufu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba tunalo eneo katika Wilaya ya Sengerema kule kwa mwenzangu Ndugu yangu Eric Shigongo tunaeneo la Kichangani ambalo linatumika kwa ajili ya uvuvi. Jimbo la Sengerema linapata samaki kutoka katika eneo hilo.

Je, Serikali iko tayari kutuachia lile eneo likaondoka katika *game reserve* kwa sababu linatoa usumbufu watu walioko pale wanalipa kama wako nchi nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na tatizo la mamba na si sehemu ya Sengerema peke yake, ni maeneo mengi ambayo yana mito na maziwa na Serikali imeendelea kujenga vizimba vya mfano. Lakini tunaelekeza pia Serikali za Mitaa tushirikiane nao ili kuhakikisha maeneo haya tunayaimarisha vizuri na wananchi waweze kupata huduma bora ya maji na pia tutashirikiana na Wizara ya Maji ili kuona kwamba wananchi wanaweza kupata maeneo mazuri ya kuchota maji badala ya kutumia maeneo ambayo yanawanyama wakali na waharibifu hususani mamba.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, swali lingine ameongelea kuhusu eneo la Kichangani; eneo hilo liko katikati ya pori ambapo ni hifadhi na tuliweza kuwaruhusu wavuvi waweze kulitumia kwa utaratibu maalum kwa sababu tunatunza mazalia ya samaki na uhifadhi mbalimbali, hivyo nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba eneo hili liko *purposefully* kwa ajili ya uhifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Igalula sasa aulize swali lake.

Na. 157

### **Baadhi ya maeneo ya hifadhi kutumiwa na wananchi**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza maeneo kutoka kwenye hifadhi katika Jimbo la Igalula ili wananchi wa Igalula wapate maeneo ya kuchungia na makazi kwa kuwa idadi ya watu na mifugo imeongezeka?

**SPIKA:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 Serikali ilifanya mapitio ya mipaka ya msitu wa Uyui Kigwa - Rubuga uliopo Igalula, Wilaya ya Uyui ambapo hekta 36,709 zilitolewa kwa ajili ya vijiji vya Matanda, Sawmill, Kalemela, Itobela, Ibelamilundi, Isenegezya na Isikizya.



**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni haja tena ya kumega eneo hilo kutoka kwenye hifadhi kwa ajili ya kuwagawia wananchi kutokana na umuhimu wa hifadhi hii kiikolojia. Aidha, vijiji vinaelekezwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuepuka migogoro mipya kujitokeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Protas Daud, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo yatakwenda kuzua mgogoro mwingine; katika vijiji alivyovitaja hapo ni kijiji kimoja tu ambacho kipo kwenye Jimbo la Igalula. Kuna Kamati ya Mawaziri nane ilikuja kule na ikatoa maelekezo kuwa itaenda kugawa maeneo katika maeneo haya, lakini katika jibu lake wanasema hawaoni haja.

Je, Serikali haioni sasa kuweka kauli inayoeleweka kwa wananchi ili waweze kutoa mkanganyiko ambao unajitokeza?

Swali la pili, Jimbo la Igalula limezungukwa na vijiji vingi vyenye mgogoro kama huu hasa katika Kata ya Miswaki, Loya, Igudi, Mwamabondo na vijiji vingine. Je, Serikali haioni haja ya kwenda kupitia mipaka upya ili kila mwananchi ajue ni wapi anaishia na hifadhi inaishia wapi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**11 NOVEMBA, 2022**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kauli ya Serikali iweke kauli sahihi kuhusiana na vijiji vilivyotajwa; kuna mapori matatu yapo ndani katika Jimbo la Igalula, kuna Pori la Iwembele, Uyui, Kigwa, Lubuga, kuna Nyahua.

Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Mbunge la msingi halikuhainisha ni vijiji gani hasa ambavyo analenga. Lakini nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la Igalula kwa maana ya Jimbo la Igalula kuna vijiji ambavyo vinaenda kunufaika na Kamati hii ya Mawaziri nane, kuna kijiji cha Miswaki, Igudi, Mwamdalaigwe, Loya na Mwamabondo, vijiji hivi vinatoka katika Jimbo la Igalula na vitaenda kunufaika na kumegewa kwa maamuzi ya Kamati ya Mawaziri nane.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuonesha mipaka, niwatoe wasiwasi Wabunge pamoja na Mbunge aliyeyuliza swali kwamba kwa utaratibu tulionao sasa ni kuhakikisha kwamba yale mapori mapya ambayo tutayapa GN mpya tutaweza kushirikisha wananchi namna ya kutambua mipaka mipya na yale ambayo yatatangazwa na Serikali kwamba haya sasa ni mapori halali basi wananchi watafahamu mipaka yao ili iwe rahisi kutoingiliana tena na kuanzisha migogoro mipya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza

**11 NOVEMBA, 2022**

nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna alivyojibu swali la Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, labda nijibu kwa ujumla kulingana na changamoto iliyokuwepo katika maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ameridhia kati ya vijiji 975, vijiji 920 wamekubaliwa kubaki kwenye maeneo yao. Kitakachofanyika ili kuondoa hizi changamoto ni ushirikishaji wa wananchi katika maeneo watashirikishwa wote na wataalam wote watakuwepo na katika maeneo ambayo tumekwishapita tayari wapo ili kuweza kubaini mipaka kwa pamoja. Na hii inafanyika hivyo ili baadae kusijekutokea lawama pengine kwamba hawakushirikishwa katika kubainisha mipaka mipya.

Kwa hiyo, tunaimani maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ameridhia na ameongeza hata pale ambapo alikuwa amesema kwamba wangeishia, imewapa pia fursa ya kuwa na maeneo ya akiba ya wao pia kuweza kuyawekea mpango wa matumizi ambao Serikali itafanya kwa kushirikiana na wao ili basi wasiendeleo kuwa na ugomvi na hifadhi ambazo ziko zimetengwa kwa kazi maalum.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na Serikali kuwapatia majibu. Nitawaletea matangazo niliyo nayo hapa kabla hatujaendelea na ratiba. Tutaanza na tangazo la wageni.

**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko Jukwaa la Spika, ni wageni wanne wa Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, Naibu Waziri wa Nishati kutoka Bukoba, Mkoani Kagera ambao ni Ndugu Majaliwa Jackson, kijana Wakitanzania shujaa aliyejitolea...*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nisome maelezo kuhusu yeye. Huyu ni Ndugu Majaliwa Jackson, kijana shujaa wa Kitanzania aliyejitolea kuokoa wahanga wa ajali ya Shirika la Ndege la *Precision* naye ameambatana na Ndugu Shaban Mkungilwa ambaye ni Sajenti wa Jeshi la Zimamoto. *(Makofi)*

Lakini pia yupo Mchungaji Peter Barnaba na Ndugu Godfrey Mwenezi, karibuni sana Bungeni na tukushukuru kijana wetu kwa kazi nzuri ulioifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba uchunguzi unaendelea, lakini lazima tutambue juhudi za kijana huyu zilizofanyika. Lakini pia na yeye natambua wazi kuwa kwamba amekuja hapa kwa niaba ya kundi kubwa la wavuvi walioshiriki katika zoezi la kuokoa wahanga hawa na pia kusaidia kutoa miili ya marehemu ambao wao hawakubahatika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunakushukuru sana kijana wetu, lakini pia tunapokushukuru wewe tunawashukuru pia wale ambao walikuokoa wewe kutoka kwenye ndege baada ya kuzimia nao tunawashukuru sana na pia tunawashukuru wavuvi wote na wananchi wote ambao walikuwa eneo hilo la karibu ambao walitoa msaada wa haraka kabla ya vyombo vyetu vya uokozi havijafika. Kwa hiyo

**11 NOVEMBA, 2022**

tunawashukuru sana wananchi wote wa maeneo hayo walioshiriki katika zoezi hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo hivyo nichukue fursa hii pia kuwashukuru sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri waliyoifanya katika zoezi zima lililotokea baada ya ajali hii kutokea. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu namna ambavyo alienda kwenye eneo hilo kwa haraka na yeye kwenda kujionea kule namna ambavyo walikuwa wakifanya hiyo kazi, lakini pia kuwashukuru wananchi kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua mbalimbali ambazo naye alizichukua ikiwa ni pamoja na kuagiza kwamba kijana huyu Majaliwa na yeye aingie kwenye Jeshi la Zimamoto na hivyo awe anasaidia na akishapata mafunzo sasa nadhani atapangiwa kitengo maalumu kabisa kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua aliyoichukua. Sasa tunawashukuru mnaweza kuketi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia pamoja na mambo mengine tunampongeza Mama Mzazi wa Majaliwa Jackson kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kumlea kijana huyu katika hali ya kumpa ujasiri na kujiamini. Kwa hiyo amefanya kazi nzuri pamoja na mazingira aliyonayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawaleta kwenu wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; tunao

## 11 NOVEMBA, 2022

wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambaye ni Waziri wa Madini na hawa ni wapiga kura wake kutoka Bukombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ,tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wanakwawa ya Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Mburahati Jijini Dar es Salaam, karibuni sana.*(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa Naibu Waziri wa Madini ambao ni viongozi wa CCM kutoka Longido, Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni wapiga kura wake kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Maryam Omar ambaye ni wifa yake kutoka Konde, Kaskazini Pemba, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim Said ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani ambao ni viongozi wa CCM Wilaya kutoka Chato, Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Aloyce Kwezi ambao ni wadogo zake kutoka Nzega, Mkoa wa Tabora karibuni sana. *(Makofi)*

## 11 NOVEMBA, 2022

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambao ni Wenyeviti wa Umoja wa Walimu Wakuu Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 38 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni viongozi wa UVCCM Tawi la SUA Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambao ni walimu kutoka Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambao ni wapiga kura wake kutoka Mabwepande, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda, ambao ni Walimu Wakuu kutoka Manispaa ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 19 wa Mheshimiwa Salim Hasham ambao ni Watendaji wa Kata na Afisa Utumishi kutoka Ulanga, Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni leo.

Sasa kabla hatujaendelea na ratiba yetu, tunalo tangazo lingine na tangazo hili linatoka kwangu na linahusu kuanzishwa kwa Bunge Bonanza.

**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukishiriki mabonanza ya taasisi mbalimbali ambazo huwa zinakuja kushirikiana na Wabunge na pia watumishi wa Bunge na sasa tunaanzisha bonanza la kwetu kama Bunge na hili litaitwa Bunge Bonanza na hili haliondoi uwepo wa yale mabonanza mengine ya taasisi, lakini Bunge kama Bunge tutakuwa na Bonanza. *(Makofi)*

Bonanza hili tofauti na hayo mabonanza mengine litakuwa linahusisha Wabunge wote na sio Wabunge tu wanamichezo, lakini pia litakuwa linahusisha watumishi wote. Sasa tunaposema wote ni kwamba kila Wabunge watasema ni mchezo gani wanaumudu wao, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mkuchika naye atasema anaweza mchezo gani na Mheshimiwa Lukuvi naye atasema anaweza mchezo gani? *(Makofi)*

Kwa hiyo siku hiyo ya Bonanza wote tulioko humu ndani na ambao hawapo wote tutakuwepo viwanjani. Kila mtu atacheza mchezo ule ambao anatakiwa kucheza na vivyo hivyo kwa watumishi wote itakuwa ni watumishi wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunatarajia Bunge Bonanza lifanyike kila robo ya mwaka mara baada ya kuhitimisha Vikao vya Kamati na sio Vikao vya Bunge. Tukishahitimisha Vikao vya Kamati kila robo mwaka tutakuwa na hili Bonanza, kwa hiyo ni muhimu kulifahamu. Hata hivyo Bonanza mojawapo kati ya hayo Mabonanza manne litakuwa ni kubwa zaidi kwa sababu hili litakuwa linafanyika kipindi cha Bunge la Bajeti na hili halitafanyika baada ya kumaliza Kamati, lakini litapangiwa tarehe maalumu kabisa ambalo Waheshimiwa Wabunge wote tutakuwa tayari kwa ajili ya Bonanza hilo.



**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, ili kufanikisha hili tutakuwa tukiwasiliana na taasisi mbalimbali na nyingine ni zenu Waheshimiwa Wabunge ili muweze kushiriki kwanza kwenye hii michezo, lakini pia kushirikiana na Bunge katika mambo mbalimbali yatakayohusu Bonanza letu. Pia tutatoa fursa kwa taasisi vilevile upande wa Serikali kama kipindi hicho watakuwa na ujumbe wowote ambao wanatamani ufike kwa wananchi, basi tutaufikisha kwa nguvu hiyo ya Bunge Bonanza.

Waheshimiwa Wabunge, tunapozungumzia Bunge Bonanza ni tofauti na *Bunge Sports Club* kwa sababu *Bunge Sports Club* inahusu wanamichezo, ni ya Bunge zima sawa, lakini inahusu Wabunge wanamichezo. Hata hivyo Bunge Bonanza ni la Wabunge wote na wafanyakazi wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo ili kuweza kutekeleza majukumu hayo ya Bunge Bonanza ili maandalizi yake na mambo yaende vizuri, basi hapa wako viongozi ambao watatoka upande wa watumishi wa Bunge na wako viongozi ambao watatokana nanyi Wabunge.

Kwa upande wa Bunge nimewateua Mheshimiwa Saada Mansour Hussein – atakuwa ni Katibu wa Bunge Bonanza na Mheshimiwa Festo Richard Sanga – atakuwa Mwenyekiti wa Bunge Bonanza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Naambiwa kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kutoka Kigoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge sasa tutaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

**11 NOVEMBA, 2022**

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Haya kuna miongozo miwili, Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni namba 76 halikadhalika Mbunge yeyote anaweza kusimama na kuomba mwongozo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Naibu Waziri swali ambalo niliuliza namba 149 ametoa majibu ambayo hayaendani kabisa na uhalisia wa swali la msingi lililoulizwa. Nilikuwa napenda kufahamu mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa uliyotoa hapo awali kuhusiana na kijana shujaa Ndugu Majaliwa Jackson, nilikuwa naomba utoe Mwongozo kama haitokuwa jambo zuri sana endapo Bunge lako ukalielekeza likaazimia kukubali tuchange shilingi 50,000 kutoka kwenye posho yetu ya siku ya leo ya kikao ili tuweze kumpa kama ishara na alama ya kutambua mchango wake mkubwa na ujasiri aliouonesha kwenye kuokoa maisha ya ndugu zetu wahanga wa ajali ya *Precision Air* iliyotokea wiki iliyopita.

Mheshimiwa Spika, naomba utoe mwongozo wako kuhusu jambo hili.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nilisimama kuhusu mwongozo, lakini hukuniona.

**SPIKA:** Haya nitakupa nafasi.

**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso kwa kutumia Kanuni ya 76 akiomba Mwongozo kuhusiana na majibu yaliyotolewa kwa swali lake namba 149, kwamba majibu yaliyotolewa hayaridhishi kwa sababu yalikuwa ni majibu ya swali la msingi na mimi niliyasoma hapa mbele.

Swali lililoulizwa lilikuwa linahusu kikingaradi lakini Mheshimiwa Naibu Waziri majibu yake yameeleza kuhusu mipango ama kazi ambayo Serikali huwa inafanya kwenye miundombinu ya nishati ikipata athari hizo za radi.

Kwa hiyo, Mwongozo wangu ni kwamba swali hilo litaulizwa upya katika Bunge lijalo na Serikali italeti majibu. Kwa hiyo huo ndio Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kigwangalla anasema anaomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 76 na kanuni hii huwa inataka kwanza jambo liwe limetokea mapema hapa Bungeni, kwa hiyo ni sawa, lakini la pili, ukiwa unataka kujua kama hilo jambo ni sawa sawa ama sio sawa sawa. Sasa hapa jambo la michango halijajitokeza kwa hiyo huwezi kuniuliza mimi nitoe Mwongozo kwenye hoja hiyo.

Mheshimiwa Kigwangalla kwa kutumia kanuni zetu kama alikuwa anakusudia kufanya hicho alichokifanya alipaswa atoe hoja, Waheshimiwa Wabunge muunge mkono halafu tuendele. Sasa kwa sababu hakufanya hivyo na mimi ameniomba mwongozo kwenye jambo hili, mwongozo wangu ni kwamba kwa sababu kijana yuko hapa Bungeni, wote mmemuona na wote mmempungia mkono, wahudumu wakati Mheshimiwa Waziri atakuwa akizungumza watapita huko kwenye madawati yenu

**11 NOVEMBA, 2022**

toeni michango apewe kijana wetu. Hapo itakuwa ni jambo la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Francis Mtinga akisema na yeye alikuwa amesimama kabla, tutamaliza na huyo ili wasianze kuamka wengine tena. Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 76 wakati ukimpongeza kijana Majaliwa, ulimpongeza pia mama yake mzazi. Tunaomba Mwongozo kwa kuwa hukumpongeza baba yake jambo hili linatupa shida sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Francis Mtinga, yeye kama ameuona mchango wa baba yake, yeye ampongeze huyo baba yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mtinga nakupa dakika moja mpongeze baba yake kijana. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi naomba kwa niaba ya Wabunge na Bunge lako nimpongeze...

**SPIKA:** Ngonja Mheshimiwa Mtinga, subiri kwanza. Anayeruhusiwa kwa niaba ya Bunge ni Spika, wewe binafsi kama Mbunge, mpongeze baba yake kijana sio kwa niaba ya Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba nimpongeze sana baba yake na kijana Majaliwa kwa malezi mazuri ambayo amempatia

**11 NOVEMBA, 2022**

kijana na kumfanya kuwa shupavu sana.  
(Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Haya dakika yako imekwisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya mambo mengine yanaweza kujadiliwa nje ya hapa. Nafikiri hili jambo liko dhahiri shahiri, wala halihitaji maelezo ya kwenda kutafuta sijui wapi ambapo pamejificha. Vilevile kijana hana fursa humu ndani ya kueleza, lakini pia namshauri aendelee na utulivu akafanye hayo ambayo amepewa fursa ya kuyafanya, wala asiingie hapo kati kati ya wazazi wawili. Mimi nimempongeza mama yake kwa sababu maalum. (Makofi)

Nimesema hivi nimempongeza mama yake kwa sababu maalum na habari ya baba amekwishapongezwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mkalama (Singida Mashariki). Kwa hiyo, tusije tukachanganya mambo hapa. Bunge limempongeza mama. (Makofi)

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere nilishasema mwongozo wa Mheshimiwa Mtinga ndio ulikuwa wa mwisho.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Jambo maalum.

**SPIKA:** Halihusu jambo hili?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Sawa, ndio.

**11 NOVEMBA, 2022**

**SPIKA:** Usiseme sawa, halihusu jambo hili?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo tulikuwa tunahitaji huyu kijana aje hapa, sisi tuko tayari kutoa tamko hela zetu zikatwe kule ili apewe kwa sababu kwa *style* hii hatapewa vizuri.

**SPIKA:** Hujatoa hoja na haijaungwa mkono. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

### **TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano wa Tisa wa Bunge sasa zimemalizika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge hiyo ndiyo Taarifa ya Katibu wa Bunge tunanendelea. Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:**

### **HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Hoja ya Kuahirisha Bunge.

**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aje atoe Hoja ya Kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, leo tunapoelekea kuhitimisha shughuli za Mkutano wa Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na uzima. Kadhalika tuendeleo kumuomba na kumtegemea Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema atujalie mafanikio zaidi katika kutekeleza majukumu yetu ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge hili tukufu, hususani Mkutano huu wa Tisa unaohitimishwa leo. Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kwamba uongozi wako umeendelea kushuhudia weledi wako, busara zako, uzoefu wako na uwezo mkubwa ambao umekuwa chachu katika kulifanya Bunge hili la Kumi na Mbili kuwa miongoni mwa mabunge bora.

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika wa Bunge hili la Kumi na Mbili ambaye kutokana na uzoefu mkubwa alionao ameendelea kushirikiana vyema na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga – Mbunge na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge katika kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu hili tukufu.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao, maoni na ushauri walioutoa wakati wa mijadala na hoja mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa mkutano huu. Hoja za Waheshimiwa Wabunge zitasaidia sana Serikali kuimarisha utendaji wake katika kuwahudumia wananchi. Hivyo basi nawahakikishia kwamba Serikali imepokea michango yenu na inaahidi kuifanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Septemba hadi Novemba, 2022 wapo Watanzania wenzetu waliopatwa masahibu mbalimbali yaliyosababisha kuondokewa na wapendwa wao, lakini majeruhi na uharibifu wa mali nao pia ulijitokeza. Hivyo basi nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako Mheshimiwa Spika kufuatia kifo cha Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani kutoka Chama cha Mapinduzi kilichotokea nyumbani kwake Zanzibar siku ya tarehe 13 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao kufuatia ajali za vyombo vya usafiri ikiwemo ajali ya ndege ya Shirika la *Precision Air* iliyotekea Mjini Bukoba Mkoani Kagera siku ya tarehe 6 Novemba, 2022 na kugharimu maisha ya watu 19. Chanzo cha ajali hii tutakuja kupata taarifa kufuatia uchunguzi unaoendelea hivi sasa na timu maalumu chini ya Wizara ya Uchukuzi. Nami niungane tena na Watanzania wenzangu nanyi Waheshimiwa Wabunge kurudia tena kuwashukuru sana makundi mbalimbali ambayo yameshiriki katika shughuli ya uokozi wakiwemo wavuvi waliokuwa jirani na tukio ambao pia kijana wetu Jackson Majaliwa ambaye tuko naye hapa alikuwa miongoni mwao, watumishi wa



## 11 NOVEMBA, 2022

uwanja wa ndege, vyombo vya ulinzi na usalama, wadau wa sekta binafsi ambao wameshiriki, madaktari na wauguzi, msalaba mwekundu, skauti, UVCCM Bukoba Mjini, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, wananchi wa mji wa Bukoba, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia alitoa maelekezo kwa kijana shujaa Majaliwa kujiunga na Jeshi la Uokozi kutokana na umahiri wake ili apate uzoefu zaidi na kijana leo yuko hapa akiwa safarini kwenda chuoni.

Pia natoa pole kwa salamu za rambirambi kwa vifo vya watu wawili waliofariki na watatu kujeruhiwa juzi tarehe 9 Novemba, 2022 kufuatia ajali ya gari iliyotokea eneo la Mlima Rwambi ikihusisha basi na gari dogo katika barabara kuu ya Mbeya kwenda Tunduma. Na huko katika kijiji cha Nabilungunya, Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara, gari la kubebea wagonjwa (*ambulance*) liligongana na Prado uso kwa uso na watu watano kupoteza maisha na watu tisa kujeruhiwa. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi na awaponye majeruhi wote kwa haraka ili waendeleo na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuimarisha utendaji ndani ya Serikali, tarehe 2 Oktoba, 2022 Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya mabadiliko kidogo kwenye Baraza la Mawaziri, kufuatia mabadiliko hayo nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). (*Makofi*)

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Mbunge, kwa kuhamishiwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge, ambaye amehamishiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwakumbusha viongozi na watendaji hususani waliopata uteuzi hivi karibuni kuzingatia suala zima la itifaki, mawasiliano, uwajibikaji wa pamoja ndani ya Serikali na kutoa ushirikiano na Bunge kama ambavyo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akielekeza na kuisitiza wakati wote. Hakikisheni kuwa katika utekelezaji wenu wa majukumu ya kila siku mnazingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaoanza mwaka 2021/2022 na unakamilika mwaka 2025/2026; bila kusahau Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu wa Tisa wa Bunge lako tukufu ulipokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka kwa Kamati za Kudumu za Bunge, maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu ya Serikali sambamba na kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge waliuliza maswali 157 ya msingi na maswali mengine ya nyongeza 440 ambayo yalijibiwa na Serikali. Hali kadhalika maswali manne ya papo kwa papo yaliyoulizwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kujibiwa baada ya kuwa ametoa taarifa muhimu za Serikali mbele ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

## 11 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu Bunge limepokea na kujadili Miswada mitatu ya Sheria kama ifuatavyo; Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa mwaka 2022; Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022; na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Tatu ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, miswada hiyo itachangia kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini na kuboresha utekelezaji wa utendaji katika kushughulikia masuala ya uwekezaji. Manufaa mengine ni kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi na masuala yanayohusiana na hayo pamoja na kuboresha baadhi ya masharti katika sheria mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia Bunge lako tukufu lilipokea na kujadili Taarifa za Kamati zinazotokana na Taarifa za Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimwa Wenyeviti wa Kamati hizo kwa mapendekezo na maazimio ya Kamati zao yaliyowasilishwa kwenye mkutano huu. Kadhalika nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao yenye tija na kujenga na ninaamini itasaidia Serikali kutekeleza mapendekezo na maazimio husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake imepokea hoja hizo na inaahidi kuzifanyia kazi na kutoa mrejesho kwa Bunge lako tukufu pindi utekelezaji wake

**11 NOVEMBA, 2022**

utakapokamilika. Na katika hatua nyingine ninaziagiza Wizara zote kuandaa taarifa za utekelezaji na ufafanuzi wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, Ofisi ya Waziri Mkuu itaandaa taarifa jumuishi ya Serikali na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Spika ikiwa ni mrejesho wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa kwa hisia na kupewa uzito mkubwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa Mkutano huu ni hoja ya ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Nyote mtakubaliana na mimi kwamba lengo la mjadala huu lilikuwa ni kutafuta suluhu ya takribani wanafunzi 28,000 wenye uhitaji wakupata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka huu 2022/2023 ambao walikuwa hawajapangiwa mikopo kutokana na ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nalishukuru Bunge lako tukufu kwa kuibua hoja zenye lengo la kuboresha utenda ji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na mfumo mzima wa ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini. Aidha, katika hatua nyingine Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia wanafunzi wote waliokidhi vigezo vya kupata mikopo waende vyuoni kuendelea na usajili kwa maelekezo ya Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la Mheshimiwa Rais ni kuwanufaisha wanafunzi wote wenye uhitaji waliopata udahili na wenye vigezo vya kupata mikopo. Katika mapitio ya bajeti ya nusu ya mwaka baadaye mwaka

**11 NOVEMBA, 2022**

huu tutaliomba Bunge lako tukufu liridhie matumizi ya fedha zitakazohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Serikali imeyapokea kwa mazingatio makubwa maoni ya Waheshimiwa Wabunge na maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Kudumu ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni tarehe 5 Novemba, 2022 kuhusu kuifanyia ukaguzi wa kina Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika mchakato mzima wa ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu hapa nchini. Hivyo basi mara baada ya timu hiyo kukamilisha jukumu hilo taarifa yake itakuwa sehemu ya nyaraka muhimu kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutekeleza maazimio ya Bunge kuhusu ukaguzi na ufanisi katika ugharamiaji wa elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninaomba msichoke kutushauri kuhusu namna bora zaidi ya kugharamia elimu ya juu nchini ili iwe endelevu, fanisi na yenye tija.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2023/2024; katika Mkutano huu wa Tisa Bunge pia lilipokea, kujadili, kushauri na kupitisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Bajeti ya Serikali unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ninatumia fursa hii kuwaelekeza Maafisa Masuuli wote kuhakikisha wanafanyia kazi hoja, ushauri na maoni pamoja na mapendekezo ya Bunge lako tukufu katika kipindi hiki ambacho maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuainisha

**11 NOVEMBA, 2022**

vipaumbele muhimu ambavyo vinaendelea. Kadhalika niendeleo kuwasisitiza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa kuhakikisha wanafanya kaguzi za mara kwa mara za matumizi ya fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakisha kuwa miradi hiyo inaakisi thamani ya fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia mwenendo wa mwelekeo wa mvua katika msimu huu wa 2022/2023; tarehe 2 Septemba, 2022 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania litoa utabiri wa mwelekeo wa hali ya hewa ya unyeshaji mvua katika msimu wa vuli kwa maeneo yanayopata mvua za misimu miwili kwa mwaka huu. Utabiri huo ulieleza kuwa katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2022 mvua za vuli zinatarajiwa kuwa mvua za chini ya wastani hadi wastani na zilizotarajiwa kuchelewa na kuwa zenye mtawanyiko usioridhisha kwa shughuli za kilimo na kuambatana na vipindi virefu vya ukavu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inaweza kusababisha upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo na kuathiri ukuaji wa mazao hasa mazao ya chakula ikiwemo mahindi na mpunga hususani katika maeneo yanayopata mvua za misimu miwili kwa mwaka. Kutokana na hali hiyo ni vema wadau wote wa masuala ya kilimo kuanza kuchukua tahadhari dhidi ya upungufu wa mazao ya chakula na kuhifadhi chakula cha kutosha mpaka hapo hali ya hewa itakapoanza kupata mvua ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Novemba, 2022 unyeshaji wa mvua katika maeneo mengi yanayopata mvua hizo hasa mikoa ya Pwani, Dar es salaam, Tanga, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro na Manyara ni wa

## 11 NOVEMBA, 2022

kusuasua. Kwa upande wa Mikoa ya Kagera, Geita, Mara na Mwanza mvua za vuli zinaendelea kunyesha na mazao ya chakula shambani yapo katika hatua mbalimbali za ukuaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauri wadau wote wa sekta ya kilimo katika kukabiliana na hali ya ukame na kuchelewa kuanza kunyesha mvua za msimu 2022/2023 kutekeleza yafuatayo:-

(i) Wakulima waendeleo kutumia mbinu bora na himilivu kwa ajili ya kilimo endelevu kinachohimili ukame na chenye ufanisi mkubwa ikiwemo matumizi ya mbolea za mboji, samadi, kilimo cha mtandazo ambacho huimarisha uhifadhi wa maji na unyevunyevu kwenye udongo, lakini pia kupanda mbegu za mazao ya chakula yanayokomaa kwa muda mfupi na kutumia maji vizuri kwenye skimu za umwagiliaji.

(ii) Maafisa Ugani endelee kushirikiana na vituo vya utafiti vilivyopo kwenye maeneo yenu kwa lengo la kupata na kusambaza teknolojia za uzalishaji wa mazao shambani. Lakini pia kufuatilia kwa ukaribu taarifa za mara kwa mara kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ili kuwa na wigo mpana wa kuwashauri wakulima kuhusiana na hali ya hewa na aina ya kilimo kinachohitajika kwa wakati huo.

(iii) Kuendelea kutoa huduma za ugani kwa kuzingatia mwongozo wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabia ya nchi, *Climate Smart Agricultural Guideline* 2017 kwa kilimo himilivu.

(iv) Tuendeleo kutumia chakula kilichopo sasa kwa uangalifu mkubwa, kuhifadhi chakula cha kutosha katika

## 11 NOVEMBA, 2022

ngazi ya familia na kuepuka matumizi mabaya ya chakula au yasiyokuwa ya lazima kama vile utengengenezaji wa pombe na matumizi ya chakula katika sherehe zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni hadi Julai, 2022 Serikali ilifanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula msimu wa 2021/2022 ili kubaini upatikanaji wa chakula nchini kwa mwaka 2022/2023. Tathmini hiyo ilionesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula unatarajiwa kufikia kiasi cha tani 17,403,880. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2022/2023 ni kiasi cha tani 15,073,855, kwa kulinganisha uzalishaji na mahitaji nchi inatarajiwa kuwa na kiwango cha utoshelevu wa kiasi cha 115%.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2022 Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilifanya tathmini ya kina ya hali ya upatikanaji wa chakula kwa ngazi ya kaya katika maeneo ambayo yalibainika kuwa upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2021/2022 na kutokana na matokeo ya tathmini hiyo Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula (NFRA) imetenga jumla tani 4,572,300 za chakula kwa ajili ya kupeleka kwenye maeneo yenye changamoto ya uapatikanaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2022 jumla ya Halmashauri 20 zimepelekewa chakula kama ifuatavyo; Liwale tani 200; Nachinwea tani 100; Bunda tani 400; Geita TC tani 100; Nzega tani 300; Sengerema tani 300; Monduli tani 100; Ngorongoro tani 100; Butiama tani 100; Meatu tani 100; Kishapu tani 100; Longido tani 1,872; Urambo tani 100; Handeni tani 100; Mkinga tani 100;



## 11 NOVEMBA, 2022

Chemba tani 100; Chamwino tani 100; Mbulu tani 100; Mwanga tani 100; na Wilaya ya Hai tani 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu wa hali ya upatikanaji wa chakula hususani mazao ya nafaka na kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kupeleka chakula kutoka Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(NFRA)* kitakachouzwa kwa bei ya chini ya bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie utendaji kazi na uwajibikaji, suala la nidhamu, utendaji na uzalishaji kwa ubora, kuzidisha weledi na matumizi sahihi ya fedha za umma kutokuwa na wataalamu wa kutosha, mifumo sahihi ya kielektroniki nalo limeibuliwa wakati wa hoja kuhusu Taarifa za Kamati zinazotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hususani kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha, kuimarisha na kuweka mifumo imara ya usimamizi wa rasilimali watu na utendaji kazi wa watumishi wa umma na taasisi za umma lengo ni kuhakikisha kuwa mifumo iliyopo na inayojengwa inasaidia kuhakikisha utendaji kazi na usimamizi wa watumishi na inakuwa na taarifa sahihi kwa lengo la kuongeza tija na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa rasilimali watu, utendajikazi na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utumishi wa umma Serikali imejenga mifumo ifuatayo; Mfumo Mpya wa Taarifa ya Kiutumishi na Mishahara.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, mfumo mpya wa taarifa za kiutumishi na mishahara ambao ulianza kutumika rasmi mwezi Mei, 2021 kuwa ni sehemu ya mfumo ambao umejengwa. Mfumo huo umeunganishwa na mfumo wa PSSSF kwa ajili ya kubadilishana taarifa za michango ya watumishi na nyaraka za hitimisho la ajira. Mfumo wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ajili ya kubadilishana taarifa za mikopo ya elimu ya juu kwa watumishi; lakini pia Mfumo wa *Ajira Portal* kwa ajili ya kubadilishana taarifa za waajiriwa wapya na Mfumo wa *NIDA* kwa ajili ya kubadilishana taarifa za utambalisho wa Taifa wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa taasisi za umma 445 zimeunganishwa na zinatumia mfumo mpya wa taarifa za kiutumishi na mishahara ili kupunguza muda wa kuchakata malipo ya mishahara kutoka siku 14 hadi siku moja pamoja na kuwa taarifa sahihi za watumishi wanaotarajia kustaafu.

Mheshimiwa Spika, mfumo huo unasimamiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuendelea kusimamia waajiri na kuhakikisha wanaingiza taarifa na nyaraka zote zilizo muhimu za watumishi kwenye mfumo mpya wa taarifa za kiutumishi na mishahara.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa pili ni mfumo wa kusimamia utendaji kazi wa watumishi wa umma na mfumo wa kusimamia utendaji kazi wa taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, mfumo mingine iliyojengwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za upimaji wa utendaji kazi wa watumishi na mikataba ya utendaji kazi wa taasisi ni mfumo wa kusimamia utendaji kazi wa

**11 NOVEMBA, 2022**

watumishi wa umma pamoja na mfumo wa kusimamia utendaji kazi wa taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mifumo hiyo mipya umekamilika, hivi sasa inafanyiwa majaribio na inatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kw amajaribio na kutoa mafunzo kwa watumishi katika taasisi zote za umma.

Mheshimiwa Spika, hatua ya mifumo hiyo kuwa ya kielektroniki itawaondoa muhali, hisia na kupendeleana au kuoneana katika usimamizi wa utendaji kazi na itahamasisha uwajibikaji wa hiari kwa watumishi wa umma itakayosaidia utoaji huduma na kwa wakati kwa umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hoja zilizoibuliwa wakati wa kujadili taarifa za Kamati zinazotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni maombi ya vibali vya ajira vya kutokuwepo kwa watumishi wa kutosha na hivyo kuathiri tija na ufanisi uliokusudiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwarobaini wa changamoto hiyo ni ujenzi wa mfumo wa tathmini ya hali ya rasilimali watu katika utumishi wa umma ambao umekamilika na tayari waajiri wote 528 wanaendelea na zoezi la kujaza taarifa za taasisi za watumishi kwenye mfumo. Mfumo huo utaondoa changamoto ya baadhi ya taasisi za umma kuwa na watumishi wengi kuliko mahitaji yao halisi au watumishi wachache kuliko inayohitajika na wakati mwingine watumishi kurundikana katika kituo kimoja kuliko mahitaji.

**11 NOVEMBA, 2022**

Mheshimiwa Spika, vilevile mfumo huo utawezesha Serikali kupata taarifa sahihi idadi ya mgawanyo wa watumishi katika taasisi za umma na maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kuhakiki, kuainisha na kuandaa mahitaji halisi ya watumishi kwenye taasisi zote za umma.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa matumizi ya mifumo ni mageuzi makubwa katika usimamizi wa watumishi na utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati nikienlekea kuhitimisha hotuba yangu, yako mambo ambayo ningependa kuyatolea msisitizo na uhifadhi wa usimamizi wa mazingira, changamoto ya maji katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, utekelezaji wa mwangozo wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 na magonjwa yasiyoambukiza. Haya ni sehemu ya maeneo yanayotiliwa mkazo katika kupanga vipaumbele vya Mpango wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nianze na uhifadhi na usimamizi wa mazingira; mabadiliko ya tabia nchi na shughuli za kibinadamu ambazo siyo endelevu na rafiki wa mazingira zimechangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa mazingira hapa nchini, ukataji wa miti hovyoy, uvamizi wa uharibifu wa mapori tengefu, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji, uchungaji wa mifugo holela pamoja na uchomaji moto misitu yetu ni miongoni mwa vitendo vinavyofanywa na sisi wenyewe bila kujali athari zake kwa mazingira yanayotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa hali hii na hali ya mazingira nchini, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika hotuba zake mbalimbali ndani na nje ya nchi

## 11 NOVEMBA, 2022

amekuwa akisisitiza kuhusu umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa jamii yetu na maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono juhudi hizo za Mheshimiwa Rais, tarehe 5 Juni, 2022 wakati wa maazimisho ya siku ya mazingira duniani ulifanyika uzinduzi wa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira. Mpango huo pamoja na mambo mengine utasaidia kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi ya mazingira nchini. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa maelekezo ya kutatua changamoto kuhusu uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Novemba, 2022 nitakutana Mkoani Iringa na Wizara zote za kisekta pamoja na Wakuu wa Mikoa ikiwemo Mikoa ya Songwe, Rukwa, Iringa, Katavi, Mbeya, Njombe, Morogoro na Pwani. Mikoa ambayo inaunganishwa na mabonde muhimu, kujadili na kuweka mikakati ya namna bora kuendeleza uhifadhi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti wa suala la mazingira ninaomba uridhie nirejee tena maelekezo niliyoyatoa kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kuhusu hifadhi za mazingira kama ifuatavyo:-

Moja; Wizara ya Fedha na Mipango ihakikshe mpango kabambe wa usimamizi wa hifadhi ya mazingira unakua sehemu ya vipaumbele vya bajeti ya kila mwaka kwa kipindi chote cha utekelezaji wake wa miaka kumi.

## 11 NOVEMBA, 2022

Pili; Wizara ya Kisekta na mamlaka ya Serikali za Mitaa zihakikishe mpango kabambe wa hifadhi na usimamizi wa Mazingira, unajumuishwa katika mipango ya bajeti zao. Sambamba na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kuwasilisha taarifa za utekelezaji, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Tatu; kila mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe maeneo yote yaliyoharibiwa yanarejeshwa kwa kupandwa miti, kusimamia vyema utekelezaji wa programu ya Kitaifa ya upandaji miti milioni 1.5 ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa ya kijani. Kudhibiti matukio ya uchomaji moto misitu na kuhakikisha maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya misitu ya mijini katika mamlaka zao hayabadilishwi matumizi wala kuvamiwa.

Nne; Wizara, taasisi, mashirika ya Kiserikali na binafsi yanayotumia nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia au shughuli nyingine za uzalishaji zianze kutumia nishati mbadala.

Tano; taasisi za utafiti na vyuo vya elimu ya juu, viendeleo kufanya tafiti za nishati mbadala ili kuondokana na utegemezi wa nishati ya kuni na mkaa katika kupikia chakula cha taasisi.

Sita; mamlaka husika zihakikishe kuwa ardhi na uoto hususan wa asili katika vyanzo vya maji, vilima na milima iliyo katika maeneo yao inalindwa na kuhifadhiwa ili kuzuia mmomonyoko wa udogo na kukauka kwa vyanzo hivyo vya maji.

Mwisho; mamlaka zinazosimamia hifadhi za wanyama pori pamoja na mamlaka nyingine zihakikishe zinadhhibiti shughuli za kibinadamu pamoja na uvamizi

**11 NOVEMBA, 2022**

katika maeneo ya mapito ya wanyama pori ili kupunguza uharibifu wa mazao, mali za binadamu, kupoteza maisha kutokana na kuwepo na mwingiliano wa wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Spika, kila mmoja katikati yetu anao wajibu wa kuhakikisha anatumiza mazingira kwani Tanzania ni mmoja tu. Nitoe wito kwa wazalishaji nchini kuendelea kuzingatia misingi ya uzalishaji endelevu, matumizi ya mbinu bora za uzalishaji na teknolojia rafiki kwa mazingira. Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuendelea kuhamasisha wananchi wetu kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha kwamba tunarejesha misitu, ekolojia na uoto wa asili katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam; kama nilivyotangulia kueleza kuwa kuendelea kwa vitendo vya uharibifu wa mazingira kumechangia ukame wa mara kwa mara na hivyo kuathiri maeneo mengi ya vyanzo vya maji kutoweka. Kwa mfano, uzalishaji katika chanzo cha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ulipungua kutoka lita milioni 520 hadi lita milioni 300 kwa siku na hivyo kusababisha upungufu wa maji katika Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam na pia katika majiji mengine kama vile Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam kuna mahitaji ya maji lita milioni 544 kwa siku. Aidha, chanzo cha Ruvu Juu na Ruvu Chini kinaweza uzalishaji kufikia milioni 520. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya ukame, uzalishaji hivi sasa ni lita milioni 300 sawa na upungufu wa lita milioni 220. Jitihada zilizofanywa kwa wiki mmoja kufufua visima 160,

## 11 NOVEMBA, 2022

tumefanikiwa kupata lita milioni 100 na kufanikisha kiwango cha uzalishaji kuwa lita milioni 400 kwa sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo hii tarehe 11 Novemba, 2022 anakabidhi mitambo ya kuchimba visima vya maji kote nchini na matumaini yetu kuwa uchimbaji utaendelea na utasaidia kupata maji ya kutosha kwenye maeneo yetu kupitia mitambo hiyo.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vikuu vya maji kwa DAWASA vinavyohudumiwa Mikoa ya Dar es Salaam na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani ni Mto Ruvu ambao huchangia asilimia 92 ya maji yote yanayozalishwa, hivyo basi kutokana na changamoto ya ukame tumeendelea kuona namna nyingine ya kupata maji ya kutosha kutoka pale tunapokabiliwa na ukame kama ifuatavyo:-

Moja; tunaimarisha matumizi visima virefu kule eneo la Kimbiji, Manispaa ya Kigamboni na Kiperu, Mkuranga.

Pili; kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba visima vya dharura vyote vilivyopo Dar es Salaam 197 vinafufuliwa na kuunganishwa kwenye mfumo wa DAWASA.

Tatu; utambuzi wa maeneo yenye uhaba zaidi wa maji kwa ajili ya uchimbaji wa visima vipya na zoezi la utambuzi linaendelea. Zoezi hilo litahusisha matumizi ya mitambo ya uchimbaji visima vilivyogaiwa leo na Rais wetu huko Kigamboni.



## 11 NOVEMBA, 2022

Nne; ujenzi wa mradi mkubwa Kidunda, mkataba wa ujenzi wa Bwawa hilo umeshasainiwa tarehe 31 Oktoba 2022; Bwawa la Kidunda likuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita trilioni 190 na ujenzi wake unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36.

Tano; mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji hadi Jijini Dar es Salaam, maandalizi ya mradi huo yameanza na utahusisha ujenzi wa mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 1,500 kwa siku ambapo awamu ya kwanza ya mradi huo itahusu ujenzi wa mtambo wa kuzalisha lita milioni 750 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya upungufu wa maji hasa katika kipindi hiki, inatokana na uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji hasa vinavyopeleka maji kwenye Mto Ruvu na kusababisha ukame kwa sababu ya uwepo wa makundi makubwa ya mifugo katika eneo la chanzo cha Mto Ruvu na vijito vyake na shughuli nyingine za kiuchumi ikiwemo uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie Mwongozo wa Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; itakumbukwa kuwa tarehe 31 Oktoba, 2022, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Sensa ya Majengo na Anwani za Makazi pamoja na Mwongozo wa Matumizi wa Matokeo ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa wananchi wenyewe, viongozi wa dini, sekta binafsi, wasanii, mtu mmoja mmoja na nirudie kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa miongoni mwa watu waliotuunga mkono kwa

## 11 NOVEMBA, 2022

kiwango kikubwa katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi kushiriki zoezi la kuhesabiwa lilioanza rasmi tarehe 23 Agosti, 2022 na kupata mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Bunge lako tukufu lilituunga mkono wakati wa kampeni ya uelimishaji na uhamasishaji wa masuala ya sensa, nitoe rai kwamba tuendeleo kuwa mabolozi wazuri wa Mwongozo wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, suala la magonjwa yasioyoambukiza; eneo lingine ambalo ningependa kulitolea msisitizo ni hali ya magonjwa yasioambukiza ambayo yameendelea kuwa tishio nchini na dunia kwa ujumla. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) magonjwa yasioambukiza yalisababisha asilimia 71 ya vifo vyote ulimwenguni kwa mwaka wa 2016.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama yalivyo mataifa mengine duniani nasi tumeathirika kwa kiasi kikubwa na magonjwa haya yasioyoambukiza kama vile kisukari na shinikizo la damu ambayo yamechukuwa nafasi kubwa yakihusishwa na matumizi ya vilevi hususan sigara na tabia bwete.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, tuunge mkono kampeni maalum ya afya, inaitwa “Afya Yangu Mtaji Wangu,” iliyozinduliwa mwaka 2016 na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kipindi hicho alipokuwa Makamu wa Rais yenye lengo la kuhamasisha ufanyaji mazoezi kama sehemu ya kupambana na magonjwa yasioyoambukiza.

## 11 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, aidha mwaka 2019 nilizindua Mpango Maalum wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasioambukiza ili kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo. Kwa msingi huo nitoe rai kwa Watanzania wenzangu kubadili mifumo yetu ya maisha, hususan kwa kushughulisha mwili na kujizuia na tabia bwete, tuendeleze mazoezi ikiwemo mchaka mchaka, mbio na riadha, michezo ya mipira ya miguu na pete, kutembea hasa mwendo wa kasi, kucheza ngoma za asili na shughuli nyingine za burudani na kijamii zinazoshughulisha mwili kama vile kulima na shughuli nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa viongozi na wakuu wa taasisi za Serikali na binafsi, oneni namna ya kutekeleza kampeni maalum ya “Afya Yangu Mtaji Wangu” kwa kufanya mazoezi katika Jumamosi ya pili ya kila mwezi ikiwa ni namna nzuri ya kuhamasisha michezo katika maeneo ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitoe wito kwa TANROADS na TARURA kuhakikisha kuwa tunapojenga barabara zetu hususan za mitaa zinakuwa chachu ya wananchi kufanya mazoezi kwa kuwa na maeneo ya watembea kwa miguu, wakimbiaji na waendesha baiskeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michezo; Waheshimiwa Wabunge sote tunajua kuwa *Bunge Sports* ipo kwenye mazoezi makali kujiandaa na Mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Sudan Kusuni kuanzia tarehe 20 Novemba, 2022. Nitumie nafasi hii kuzitakia kila la kheri timu zetu zikafanye vizuri na zirudi na makombe zaidi ya makombe waliokuja nao mwaka 2021.

**11 NOVEMBA, 2022**

Kwa upande wa michezo hususan mpira wa miguu hapa nchini, nchi yetu imeendelea kupata mafanikio makubwa, mwaka huu tumeshuhudia *Tembo Warriors* wakifika hadi hatua ya robo fainali ya Mashindano ya Kombe la Dunia ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu mwezi Oktoba, 2022 nchini Uturuki. Kadhalika, tumewashuhudia timu yetu ya Taifa ya Wasichana ya chini ya miaka 17 *Serengeti Girls* nao wakifika hatua ya robo fainali Kombe la Dunia katika michuano ya wanawake iliyofanyika nchini India mwezi Oktoba, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia *Simba Queens* ambao licha ya ugeni wao kwenye mashindano ya Klabu Bingwa ya wanawake kwa upande wa mpira wa miguu Barani Afrika wamefanikiwa kufika nusu fainali na kuondolewa na *Mamelodi Sundowns*. Ninawatakia kila la kheri katika mchezo wa kesho dhidi ya *Bayelsa Queens* kutafuta mshindi wa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza *Simba Sports Club* kwa kufanikiwa kuingia kwenye hatua ya makundi ya michuano ya Klabu Bingwa Barani Afrika. *(Makofi)*

Kipekee kabisa ninawapongeza sana *Dar Young Africans....(Makofi)*

Naomba kurudia, kipekee kabisa ninawapongeza sana *Dar Young Africans* ambao kwa mara ya kwanza wanaweka rekodi dhidi ya vilabu vya Kaskazini mwa Afrika kwa kufanikiwa kuiadhibu *Club Africain* ya Tunisia ikiwa nyumbani kwake na kutinga katika hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho kwa kishindo. *(Makofi)*

**11 NOVEMBA, 2022**

Napenda kumpongeza sana mchezaji Aziz Ki kwa kupata goli pekee ugenini, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya vizuri kwa miamba hii ya soka hapa nchini, sit u tumepata heshima na kulitanagza Taifa letu, lakini pia tunaifanya *NBC Premium League* kuwa miongoni mwa ligi bora Barani Afrika na hivyo kufuatiliwa na watu wengi zaidi duniani. Hali hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya mchezo wa soka wenye wapenzi wengi duniani sambamba na kuimarisha maslahi ya wachezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri wawakilishi hawa Watanzania katika Mashindano ya Klabu Bingwa na Kombe la Shirikisho la vilabu Barani Afrika. *(Makofi)*

Pia niipongeze Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa usimamizi mzuri na Shirikisho la Soka Tanzania kwa uratibu mzuri na ni matumaini yangu kwamba wataendelea kuratibu na kusimamia vizuri ili mchezo wetu uweze kwenda mbali zaidi. *(Makofi)*

Aidha, nitoe wito kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana kwa karibu na wadau wa michezo nchini kuhakikisha kwamba michezo na wanamichezo wetu wanapata mafanikio makubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nikiwa nahitimisha sasa hotuba yangu, namshukuru sana Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri wanayotupatia kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza majukumu yetu ya Mkutano wa Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili, lakini pia nawashukuru viongozi

**11 NOVEMBA, 2022**

na watendaji wa Serikali na taasisi mbalimbali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye mkutano huu kwa umahiri mkubwa, weledi na ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru wanahabari kwa uchambuzi mzuri wa hoja za mwenendo mzima wa Bunge na kuwahabarisha wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma nzuri kwa ushiriki wa Bunge hili. Kadhalika bila kuwasahau madereva wetu waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni na niendeleo kuwatakiwa kheri katika safari za kurejea Majimboni kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo haya, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 31 Januari 2023, siku ya Jumanne saa tatu kamili asubuhi katika Ukumbi huu hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, ndio utaratibu wetu, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

**11 NOVEMBA, 2022**

wa Tanzania ya kuliahirisha Bunge mpaka tarehe hiyo wanayoitaja waseme ndio. *(Kicheko)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa hotuba nzuri ambayo imesheheni mambo mengi na makubwa, mazito ambayo Bunge hili limeyafanya, lakini pia yamefanywa na upande wa Serikali, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niseme machache halafu tuendelee na ratiba iliyo mbele yetu.

Nianze kwanza na shukrani, nitumie fursa hii ...

Mheshimiwa Getere atafute nafasi ya kukaa akae.

Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kunisaidia, nimshukuru sana, wakati nikimshukuru yeye niwashukuru pia Wenyeviti wetu wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa David Kihenzile, ninawashukuru sana kwa usaidizi ambao huwa mnautoa siku zote. *(Makofi)*

Pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wetu wa Kamati zote za Bunge, ninawashukuru sana Wenyeviti, Makamu Wenyeviti kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa sababu kazi kubwa ya Bunge inafanyika kwenye

**11 NOVEMBA, 2022**

ngazi ya Kamati na ninyi ndio mnaongoza hizi Kamati. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya.

Lakini ni dhahiri Waheshimiwa Wabunge, kazi hiyo isingewezwa kufanywa bila ninyi kuhudhuria hizo Kamati, kwa hiyo ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mahudhurio mazuri kwenye ngazi ya Kamati na hivyo kuwawezesha Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wetu kufanya kazi nzuri na kutuletea taarifa hapa ndani kwa zile Kamati ambazo zimeleta taarifa safari hii, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu haiwezi kukamilika bila kumshukuru Katibu wetu wa Bunge pamoja na watumishi wote wa Bunge wanafanya kazi nzuri, Katibu wa Bunge tunakushukuru sana kwa namna ambavyo unasimamia utaratibu wote wa namna ya uendeshaji wa shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Pia wapo Makatibu wetu wa Kamati, tunawashukuru sana, lakini pia tunao watumishi wote wa Bunge, kwa sababu ili Wabunge tufanye kazi vizuri na Makatibu Kamati wafanye kazi vizuri wako watumishi ambao huwa wanakaa ofisini kutuwezesha kufanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana wote hao, Katibu wa Bunge utupelekee salamu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie pia fursa hii kuishukuru Serikali. Serikali nayo inatoa ushirikiano mkubwa sana kwa Bunge na hoja zenu mnazozibua kwenye Kamati, Serikali inawasikiliza na yako mazingira ambayo wanabadilisha mipango yao hapa na pale na



**11 NOVEMBA, 2022**

inapokuwa ni miswada basi wanabadili hiyo miswada kulingana na maoni yenu na maoni ya wadau ambao ninyi mnakuwa mmeyasikia na wakati mwingine mawazo yenu ambayo mnakuwa mmeyatoa kutoka kwa wananchi, Serikali inawasikiliza, kwa hiyo kwa niaba yenu, niwashukuru sana Serikali kwa ushirikiano ambao mnautoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa ushirikiano, lakini pia tunawashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri kwa namna ambavyo mnashirikiana na Waheshimiwa Wabunge kwenye ngazi ya Kamati lakini hata Mbunge mmoja mmoja anapokuja kuwaeleza hoja zao huwa mnawasikiliza, kwa hiyo tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Tunafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri, Naibu Mawaziri na ninyi kazi hizo zisingekuwa rahisi bila kuwa na watendaji kwenye Wizara zenu, tunawashukuru sana watendaji wa Wizara zote wakiongozwa na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, safari hii nafikiri tuna Bunge ni muhimu kabisa, pamoja na kwamba CAG anafanya kazi kwa niaba yetu, lakini leo kipekee kabisa tumshukuru CAG kwa kazi nzuri anayoifanya ya kufuatilia matumizi ya mapato ambayo tunapata kama fedha za umma. *(Makofi)*

Kwa hiyo tunamshukuru sana CAG kwa kazi nzuri anayoifanya lakini pia na ushirikiano anaoutoa kwa sababu Kamati zetu hizi za Hesabu za Serikali na Hesabu za Serikali za Mitaa zisingeweza kufanya kazi bila usaidizi wa CAG. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa kazi nzuri

**11 NOVEMBA, 2022**

anayoifanya na tunaamini ataendelea kufanya hivyo.  
(Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwasema hao wote kwa hizo shukurani, nitumie pia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoliongoza Taifa letu. (Makofi)

Tunamshukuru kwa sababu na yeye anatoa ushirikiano mzuri kwetu kama Bunge na hapa mmesikia taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ikieleza namna ambavyo Bunge hili lilikuja na azimio kuhusu ama tuseme Bunge lilipitisha azimio baada ya mjadala mkali sana kuhusu watoto wetu walioenda vyuoni ambao walikosa mikopo kutoka kwenye Bodi ya Mikopo. Leo mmemsikia hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu akieleza kwamba Mheshimiwa Rais ameridhia vijana hawa ambao walistahili kupata mikopo, lakini hawakupata mikopo na Bunge tukasema kwamba waende vyuoni wakati Serikali inajipanga, sasa Serikali imeshajipanga na kama mlivyosikia kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba Serikali itawalipia watoto hao hiyo mikopo inayotakiwa.  
(Makofi)

Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ushirikiano huo na Bunge letu kwa hayo ambayo Bunge linaamua na Serikali inafanya, inaweka mahusiano mazuri sana. Kwa hiyo sote kwa pamoja tumshukuru Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake yote kwamba sisi kama Wabunge na ninyi huwa mnaeda kwenye ziara mbalimbali ni mashahidi kwamba miradi yote ya kimkakati inaendelea kutekelezwa. (Makofi)

**11 NOVEMBA, 2022**

Kwa hiyo, miradi yote ya kimkakati inaendelea kutekelezwa, miradi mikubwa, miradi midogo yote inaendelea na utekelezaji na ni jambo la kumpongeza kwamba anaendelea kutafuta fedha hapa na pale ili miradi hii isisimame. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo tunafahamu anaendelea kutafuta fursa hapa na pale basi tunamtakia heri katika hayo pia ya kuhakikisha Taifa letu linasonga mbele.

Waheshimiwa Wabunge, nami niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hii hoja ya kumpongeza Rais kwa ajili ya tangazo la wananchi wa Tanzania tumeshafikia wangapi?

Ninyi Waheshimiwa Wabunge, mlifanya kazi nzuri sana na niwapongeze sana kwa uhamasishaji mkubwa mlioufanya kuhakikisha Watanzania tunahesabiwa ili baada sasa ya kuhesabiwa, hata yale ambayo huwa tunaishauri Serikali, tunakuwa tunaishauri Serikali kwa kutaja idadi ya wananchi ambao wanahitaji huduma fulani ama wanaathirika na jambo fulani. Jambo hili ni kubwa sana, tunaipongeza sana Serikali.

Pia tunaomba kwa sababu jambo hili ni endelevu kwa maana ya kwamba litaendelea kila baada ya miaka kumi, lakini sasa kipindi hiki wakati tukielekea huko kwenye miaka kumi, naamini hizi taarifa zitaendelea kuboreshwa ili nasisi tunapoendelea kuboreshwa ili na sisi tunapoendelea kuzungumza kuhusu mahitaji ya wananchi, tusigote tu hapo. Kadri tunavyoongezeka na huduma ziwe zinaongezeka vivyo hivyo na hilo naamini uwezo huo Serikali inao wa kuendelea kuboresha

**11 NOVEMBA, 2022**

takwimu zetu kadri wananchi wanavyoongezeka maana kupungua siyo kukubwa sana, kuongezeka ndiyo kukubwa maana yake, wale wanaozaliwa na vifo pia vinasajiliwa. Kwa hiyo, ni muhimu kuendelea kuweka takwimu sawasawa ili Waheshimiwa Wabunge wanapoishauri Serikali, wawe na uhakika wa yale wanayoishauri kwa kutumia takwimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema machache hayo, nami niwatakie kila la kheri Serikali yetu kwenda kuandaa sasa huu mpango ambao Waheshimiwa Wabunge wametoa mawazo yao, tunaamini kwamba kile ambacho mtatuletea mwakani, *In Shaa Allah*, Mwenyezi Mungu atuweke, kitakuwa na mawazo ya Wabunge, kitakuwa kimetazama utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025 tumefikia wapi, tunataka kwenda wapi katika hiki kipindi cha mwaka 2023/2024, lakini pia mtakuwa mmetazama Mpango wa Miaka Mitano ambao Bunge hili liliupitisha. Kwa hiyo, tunaamini hayo yote mtakuwa mnaenda kuyafanyia kazi na tunawatakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, pia niwatakie kila la kheri wale ambao tunaweza tusipate fursa ya kuonana na wanaenda huko ambako Waheshimiwa Waziri Mkuu ameshazungumza, wale watakaenda Juba kuliwakilisha Bunge hili, tunawatakia kila la kheri katika michezo na mfahamu tu kwamba mnaenda huko kwa uwakilishi, wako wengine ambao ni wazuri sana na watabaki hawataenda nanyi. Ninyi mnaoenda huko mkahakikishe kwamba mnafanya vizuri ili mtakaporejea hapa basi, kama ambavyo tulitangaza makombe mengi mwanzoni mwa mwaka huu, tunaamini kwamba tutatangaza makombe mengi zaidi mwaka huu. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri katika michezo. *(Makofi)*

**11 NOVEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, pia nawatakia Krismasi njema na Mwaka Mpya 2023, Mwenyezi Mungu atujalie sote tuje tuonane tena wakati mwingine hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kuna jambo lingine hapa, fedha ambazo Waheshimiwa Wabunge zimekusanywa kwa sababu zimekusanywa humu Bungeni tukiwa tumezungumza, kwa hiyo, ni muhimu taarifa zetu ziseme kwamba tumepata kiasi gani?

Waheshimiwa Wabunge, kiasi kilichopatikana ni shilingi 5,023,000. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu hii ambayo mmeitoa pamoja na kwamba hoja iliyokuwa imetoka na mimi sitaki kubadilisha hicho, hoja iliyokuwa imetoka ni kwamba tumchangie huyu kijana wetu, lakini kama nilivyosema, kijana huyu ana watu wale waliomuokoa na yeye wakati akiwa katika hali mbaya, kwa hiyo, anaweza akawakumbuka na hao pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nimwite Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc -KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

**11 NOVEMBA, 2022**

*(Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika  
Mashariki Ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, fedha hizi zilizokusanywa atakabidhiwa kwa niaba yetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na atamkabidhi kijana wetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa tatu kamili asubuhi siku ya tarehe 31 Januari, 2023.

*(Saa 6.15 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya  
Jumanne, Tarehe 31 Januari, 2023)*